




UKURASA 4

## MGOMBEA urais wa TLS ataja vipaumbele 10


Wajasiriamali wawa mashuaa, kujifunza matatizo kuwa fursa
Kujitokeza kufuatilia ni kufanikisha maendeleo yako
Nipashe TESA
Jumanne Mei 10, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ndivyo miji inavyotisha kiudhalilishaji kinamama
ELIMU
NA GERALD KITABU
Serikali, EU sasa kuwaonyesha Watanzania ulipo mlo wenye lishe
• Kujenga vituo vya misosi asilia Dar, Z'bar

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Mei 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580941

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wananchi wasubiri ahueni ya mafuta leo




January Makamba

UKURASA 2


Halima Mdee

# Hatima ya kina Mdee kesho

UKURASA 2



# Mbunge aja na hoja ya kuhalalisha rasmi gongo

UKURASA 3

MICHEZO PABLO AFUNGUKA TETESI KUTUA ORLANDO PIRATES UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akizungumza na mfanyabiashara wa vitambaa, Juma Hamad (kulia), walipokuwa wakitembea mitaani kuinadi Kampeni ya Teleza Kidijitali kwa Mkoa wa Dar es Salaam, iliyofanyika Tawi la Benki ya NMB Tandika jana. Katika kampeni hiyo wafanyakazi wa NMB walitembea mitaani na kutoa elimu kwa wateja kuhusu mikopo ya Mshiko Fasta, Lipa Namba na NMB Pesa Wakala na kufungua akaunti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wasubiri ahueni ya mafuta

**Jenifer Gilla na Maulid Mmbaga**

WANANCHI wanasubiri uamuzi utakaotolewa leo na serikali kuhusu njia za kuwapa ahueni ya makali ya maisha kutokana na kupaa kwa bei ya mafuta.

Leo serikali inatarajiwa kuwasilisha bungeni mikakati ya dharura iliyojiwekea katika kuwanusuru wananchi kutokana na kupanda kwa bei ya nishati hiyo, maisha ya wananchi yanazidi kuwa magumu kutokana na kuendelea kupaa kwa bei za bidhaa.

Uchunguzi wa Nipashe umeibaini kupanda kwa bei ya bidhaa ikiwamo tambi, unga wa ngano, unga wa mahindi na sabuni, kumeshika kasi baada ya kutangazwa kwa bei mpya ya mafuta ya petroli na dizeli Jumatano iliyopita.

Sharifa Hassan muuza duka la vyakula jijini Dar es Salaam, alisema kuwa wamelazimika kupandisha bei ya bidhaa hizo kutokana na kuzinunua kwa bei ya juu katika maduka ya jumla.

"Unga wa ngano namba moja wa kilo 25 sasa tunanunua Sh. 42,000 tunalazimika kuuza Sh. 1,800 kutoka Sh. 1,200 ya awali. Unga wa mahindi sasa tunauza Sh. 1,300 kutoka Sh. 1,200 kwa sababu na sisi tunanunua Sh. 27,000 kutoka Sh. 24,000 ya awali," alisema.

Alisema bei ya bidhaa nyingine ni sabuni ya jamaa ambayo katoni moja sasa wananunua Sh. 72,000 kutoka 42,000 ya awali, na kwamba wanalazimika kuuza Sh. 700 kutoka Sh. 500 kwa kipande.

Alitaja bidhaa nyingine iliyopanda kuwa ni tambi aina ya Santa Lucia ambazo wananunua Sh. 34,000 kutoka Sh. 24,000 kwa katoni ambao nao wanauza Sh. 1,900 kutoka Sh. 1,500 kwa pakiti moja.

**MAGARI YASITISHA HUDUMA**

Baadhi ya magari yanayotoa huduma ya usafiri wa abiria yamesitisha huduma hiyo kwa madai ya kupata hasara, Nipashe imebaini.

Uchunguzi huo wa Nipashe kuanzia siku za mwisho wa wiki umebaini baadhi ya wenye daladala hasa makubwa aina ya 'Eicher' wameegesha magari yao kwa madai ya kupata hasara kutokana na kupaa kwa bei hiyo mfululizo.

Imegundulika baadhi ya ruti zilizoathirika ni za kati ya Masaki na Chanika, pia Segerea na Makumbusho.

Mmoja wa wamiliki wa daladala hizo zinazotoa huduma Masaki- Chanika (jina tunalo), alisema ameamua kulaza gari nyumbani kutokana na kutoona faida tangu bei ya mafuta kupanda.

"Faida sipati tena kama zamani, kutoka kupata Sh.300,000 hadi hadi 180,000 maana gharama nyingi zinakwenda kununua mafuta, nimeona nisimame kwa muda nisikilizie upepo," alisema.

Mmiliki huyo alilalamika kwamba mabadiliko ya gharama ya mafuta ya sasa inakuwa ngumu kuendana na hesabu hiyo, huku baadhi ya magari yao bado yanamarejesho ya mikopo kwenye taasisi za fedha.

Mmoja wa madereva wa daladala hizo, Ally Athumani, alisema uamuzi wa wamiliki hao kusimamisha biashara hiyo umegeuka mwiba katika maisha yake kwa kuwa sasa hana kibarua chochote kinachomwingizia pesa.

"Sasa hivi unavyoniona nina siku ya pili sina kazi bosi kapaki gari anasema haridhishwi na tunachompelekea kwa sababu kimepungua, nina watoto wawili na mke sielewi nifanyeje, 'dayworker' (kibarua cha muda) nazo zimekuwa ngumu kwa sababu madereva wapo wengi hawana magari," alisema Ally.

**BEI ZAPAA USIKU**

Aidha, uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwa baadhi ya ruti za daladala hizo zinapandisha bei ya nauli tofauti na iliyopangwa ili kufidia bei ya mafuta.

Nipashe ilibaini baadhi ya mabasi mathalani, yanayohudumia kati ya Mbezi na Tandika nyakati za usiku yalitoza nauli ya Sh. 1,000 badala ya Sh. 850 zilizotakiwa.

Mmoja wa makondakta wa daladala hizo (jina linahifadhiwa) alisema wanatumia njia hiyo ili kufidia pesa ya mafuta na wapeleke kwa mmiliki pesa waliokubaliana.

"Ndio hivyo dadangu, hapa inabidi tukomae ili twende sawa na mwajiri, tupate hela ya mafuta na kidogo cha kwetu ili tulee familia, si unajua. Mwenye gari haelewi mwelezo anataka mzigo wake, ukimzingua anakuweka kando anampa gari mwingine," alisema.

**BUNGE LAELEKEZA**

Uamuzi wa kuwasilisha bungeni mikakati ya dharura kunusuru wananchi na kupanda kwa bei ya mafuta ulifikiwa baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, Alhamis wiki iliyopita kumwagiza Waziri wa Nishati, Januari Makamba, kupeleka majibu bungeni leo, kuhusu mkakati huo.

Mjadala huo uliibuka kufuatia Mbunge wa Kilindi (CCM) Omary Kigua, kutoa hoja ya kutaka Bunge liahirishwe kujadili suala la kupanda mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Akitoa hoja hiyo, Kigua alisema kwa sasa kuna tatizo la kupanda kwa haraka kwa mafuta kulikosababisha kupanda bei ya kila kitu na kusababisha malalamiko nchi nzima.

Alisema wabunge wana wajibu wa kusimamia na kuishauri serikali na kwamba wananchi wamewapa dhamana ya kuwasemea na kukaa kimya watakuwa hawawatendei haki wananchi.

Hoja hiyo iliungwa na wabunge zaidi ya 20 hali ilimlazimu Spika wa Bunge, Dk. Tulia kukubali ijadiliwe na wabunge.

**RAIS AITISHA KIKAO**

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan, aliitisha kikao cha dharura na baadhi ya mawaziri wahusika kujadili mafuta na kuwaagiza viongozi hao watafute suluhisho la haraka kukabiliana na hali hiyo.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria kikao hicho ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Nishati Januari Makamba, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata.

**CHADEMA YATOA NENO**

Jana, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Uenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) John Mrema, alisema Kamati Kuu ya chama hicho baada ya kukutana itapeleka taarifa kwa Baraza Kuu juu ya kupanda kwa bei ya mafuta ambao umezidisha ugumu wa maisha kwa Watanzania.

"Kamati itapeleka taarifa mahususi kwa Baraza Kuu ambalo lina viongozi kutoka wilaya zote nchini bara na visiwani na baada ya kujadili tutatoka na njia na ushauri ni hatua gani zichukuliwe kwa dharura, ili kukabiliana na hali hii ya kupanga kwa gharama za maisha kutokana na gharama za mafuta," alisema Mrema.

## Hatima ya kina Mdee rasmi kujulikana kesho

**Na Maulid Mmbaga**

HATIMA ya Halima Mdee na wenzake 18 ambao wako bungeni kwa viti maalum, inatarajiwa kujulikana kesho, kwenye kikao cha Baraza Kuu la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Uenezi wa CHADEMA, John Mrema, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ajenda za kikao cha Baraza Kuu la chama taifa linalofanyika leo.

Aidha, katika kikao hicho Kiongozi wa Chama Kikuu cha Upinzani Uganda, National Unity Platform (NUP), Bobi Wine, atahudhuria kama mgeni mwalika.

Alisema waliokuwa wanachama wao 19 ambao walishafukuzwa na kamati kuu, hivyo waliamua kukata rufani kwenye baraza kuu, na kwamba wameshaitwa kwa barua rasmi kwa ajili ya kusikiliza uamuzi wa rufani walizokata.

Wabunge hao wa viti maalum waliokata rufani ni Halima Mdee, Esther Matiko, Grace Tendega, Cecilia Pareso, Ester Bulaya, Agnesta Lambart, Nusrati Hanje, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga na Tunza Malapo, Asia Mohammed, Felister Njau, Nagenjwa Kaboyoka; wengine ni Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Stella Fiao, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

Walifukuzwa uanachama baada ya kukaidi maelekezo ya CHADEMA ya kuwataka kutoenda bungeni, kwa madai kuwa hawakuteuliwa kihalali kuwa wabunge wa viti maalum kupitia chama hicho.

Kamati Kuu ilisema kuwa uteuzi wao uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kuwa na baraka za chama.

Ajenda nyingine ni mpango mkakati wa miaka mitano ya chama pamoja na mpango kazi wa mwaka, ambao utajadili namna watakavyo kiendesha chama hicho hadi kufikia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na serikali za mitaa 2024.

"Hii ni baada ya baraza kuu kupokea taarifa ya uchaguzi mkuu wa 2020 na kwenye mpango mkakati huu ndipo tutakapojadili kwa kina masuala ya katiba mpya na tume huru ya uchaguzi na baada ya baraka kuu tutawaeleza kile ambacho tumekubaliana juu ya mambo hayo," alisema Mrema.

Aliongeza kuwa ajenda nyingine ni ratiba ya uchaguzi wa ndani ya chama akisema kuwa uchaguzi mkuu wa kuchagua viongozi wa chama ratiba yake imekaribia na baraza kuu ndilo lenye mamlaka ya kutangaza tarehe rasmi ya lini wanakwenda kuanza mchakato wake utakaoanzia ngazi ya msingi, tawi, kata, majimbo, wilaya, mikoa, kanda na kuhitimishwa kwa ngazi ya taifa.

Ajenda nyingine ni uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wadhamini baada ya kufariki kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Arkado Ntagazwa, akieleza kuwa bodi hiyo ni takwa la kisheria na mwenye mamlaka ya kuteuwa wajumbe kujaza nafasi hiyo ni baraza kuu la chama.

"Kesho Baraza Kuu litakuwa na kazi ya kuteuwa mjumbe wa bodi ya wadhamini kuziba nafasi ya mzee Ntagazwa pamoja na wajumbe wengine kadri watakavyoona inafaa kwasababu sheria ya bodi inataka wajumbe wasiopungua saba na wasiozidi tisa," alisema Mrema.

## Gwajima: Uzalishaji chuma ungeanza kisha ujenzi SGR

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, amesema kutokana na taifa kutokuwa na maono na ajenda ya muda mrefu imesababisha kuanza kwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kabla ya mradi wa kuzalisha chuma.

Akichangia jana makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/23, Askofu Gwajima alisema serikali imeanza ujenzi wa reli hiyo lakini malighafi inayotumika kwa wingi ni chuma na kuhoji ilikuwaje wakaanza ujenzi wa reli badala ya kuanza uzalishaji wa chuma ili kitumike katika ujenzi wa reli hiyo.

"Ni kitu gani kimetokea hadi kipaumbele cha kwanza kimekuwa cha mwisho na cha mwisho kimekuwa cha kwanza…kinachosumbua ni kukosa maono na mipango na dira ya Taifa, si mlaumu mtu yeyote kama kungekuwa na maono ya viwanda ya muda mrefu tungeanza na chuma tungeokoa mabilioni ya fedha," alisema.

Mbunge huyo alisema nchi inahitaji maono ama ajenda ya Taifa ya pamoja na kwamba nchi nyingi zilizoendelea zina maono ya muda mrefu.

"Katika mwaka 2018 Tanzania iliingiza chuma chenye thamani ya Dola za Marekani milioni 401.2, mwaka 2019 (milioni 491.9), mwaka 2020 (milioni 423.4) na mwaka 2021 (milioni 700.8) na mwaka 2022 (milioni 234.7), hivyo katika miaka hiyo serikali imetumia Dola za Marekani bilioni 2.2 kuagiza chuma nchini, kwa mtu mwenye akili hawezi kuruhusu jambo hili kufanyika ingali vyuma vipo nchini," alisema.

Akimpa taarifa mchangiaji huyo, Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, alisema kuna mahali taifa limeteleza kwa kufuta hata Tume ya Mipango ambayo ingetengeneza mipango hiyo.

Akiendelea kuchangia, Gwajima alisema hata makaa ya mawe yaliyogundulika zamani yanafikia ukomo wake mwaka 2030 lakini hayajatumika na kwamba Manaibu Mawaziri, Mawaziri na Rais (Samia Suluhu Hassan) zawadi watakayowapa Watanzania ni maono ya nchi.

Hata hivyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisimama kumpa taarifa mchangiaji huyo ambapo alidai kuwa nchi imekuwa ikipanga mipango na nchi nyingine zimekuwa zikiiga mipango hiyo na kutaka wasijidharau.

Akiendelea kuchangia Askofu Gwajima alisema amemsikiliza vyema na anamshukuru kwa kusema kuwa hakuna mipango ya muda mrefu ya miaka 50 wala 100.

# Mwigulu aihakikishia IMF ushirikiano na sekta binafsi

**Na Benny Mwaipaja, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amelihakikishia Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwamba serikali itashirikiana na sekta binafsi katika kuharakisha maendeleo ya nchi pamoja na kutenga kiasi kikubwa cha bajeti ya mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya kupunguza makali ya kupanda kwa gharama za maisha ya wananchi.

Dk. Nchemba amesema hayo jijini Dodoma, alipokutana na timu ya wataalamu IMF, ikiongozwa na Mshauri wa Uchumi na Fedha anayesimamia Idara ya Afrika kwenye shirika hilo, Charambos Tsangarides.

Timu hiyo ipo nchini kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya uchumi na kisera, ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa mpango wa shirika hilo wa kuipatia Tanzania mikopo na misaada zaidi ya kutekeleza miradi ya maendeleo, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kukutana na kuzungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Kristalina Georgieva, jijini Washington, Marekani, hivi karibuni.

"Miongoni mwa mambo waliyoafikiana ni kutuma timu kuja hapa nchini ili kuona namna tutakavyoshirikiana kutengeneza sera mpya za kifedha zitakazosaidia kufufua uchumi kutokana na madhara ya UVIKO-19 pamoja na vita inayoendelea baina ya Urusi na Ukraine," alisema.

Alisema kuwa maelekezo ya Rais Samia katika bajeti ijayo, ni kwamba fedha nyingi zaidi zitaelekezwa katika sekta zinazozalisha kwa wingi ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuchochea uchumi na ajira. Wakati huo huo sekta za kijamii zitaendelezwa ili kulinda rasilimali watu.

Tsangarides, alisema kuwa timu yake itaangalia uhimilivu wa Deni la Taifa pamoja na sera mbalimbali ambazo zikiboreshwa zitaleta tija katika kuinua uchumi wa nchi.

Aidha, Tsangarides alishauri kuwa programu inayoandaliwa inalenga kuongeza uwezo wa kifedha kwa Tanzania ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kulinda sekta za kijamii kama vile afya, elimu, maji, pamoja na kuboresha rasilimali watu na kuendeleza sekta binafsi.

Timu hiyo ya wataalamu itakuwapo nchini kwa muda wa majuma mawili ambapo itakutana na wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine mbalimbali.



Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete (katikati waliokaa), akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa CCBRT na wageni waalikwa katika hafla ya chakula juzi usiku jijini Dar es Salaam. CCBRT na Taasisi ya Jakaya Kikwete waliandaa chakula cha usiku kuchangisha fedha kwa ajili ya kitengo kipya cha afya ya mama na mtoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ataka gongo irasimishwe

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Momba (CCM), Condester Sichalwe, ametinga bungeni na baadhi ya pombe za gongo za nje ya nchi ambazo zinauzwa nchini, ili kuishawishi serikali kuzipima na kuzirasimisha pombe za kienyeji zilizopo nchini.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/23, Sichalwe alisema baadhi ya nchi za nje zimekuwa zikiwasaidia watu wanaotengeneza pombe za kienyeji na kuzirasimisha na ili kudhibitisha hilo amefika bungeni na baadhi ya pombe hizo za gongo ambazo zimetoka nje ya nchi ikiwamo Malawi na Zambia na zinauzwa hapa nchini.

"Watu wanaona kunywa pombe za kienyeji kuwa hawana akili lakini ukinywa bia unaonekana wa kisasa, hata katika balozi wamekuwa wakitenga fedha kwa ajili ya kununua pombe za bei ghali, lakini ukizionja hazina ladha ya tofauti na gongo,"alisema.

Aliongeza "Tunajiuliza ni kwasababu hizi zina jina la kizungu na hizi ni za kibantu. Bodi hii itakapounda itasaidia kwenda kupima viwango vya kilevi vilivyopo. TBS (Shirika la Viwango Tanzania), wanaweza kupima wakaondoa makali yaliyoko kwenye gongo ifanane na hizo pombe ambazo matajiri wanakunywa."

Mbunge huyo alisema kupitia biashara hiyo ya pombe za kienyeji wapo wafanyabiashara maarufu na wabunge wamesomeshwa na fedha zinazotokana na mauzo ya pombe hizo akiwamo Mbunge wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo.

"Wanawake wanaofanya vizuri katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ni kinamama wanaofanya biashara ya pombe za kienyeji, hatuwezi kuthamini vyetu, hata pombe hatuwezi kuwasaidia hawa watu wapate ithibati (vyeti vya ubora)," alisema.

Akimpa taarifa mchangiaji huyo, Prof. Mkumbo alisema kijijini kwake Mgela (mkoani Singida) wamejenga hadi klabu cha pombe ambacho ni moja ya vyanzo vya mapato vya serikali na kukiri kuwa mmoja wa wabunge waliosomeshwa kwa fedha zinazotokana na kuuza pombe.

Hata hivyo, akijibu hoja hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Sera na Uratibu, George Simbachawene, alisema kiwango cha ulevi kilichoko katika pombe hizo ndicho kinachoisumbua serikali na kuomba wapewe muda wa kuliangalia hilo.

"Tumekuwa tukipata hoja kama hizi zikijirudia rudia ndani ya bunge wacha tuichukue kama serikali halafu tufanye tafakari tufanye tathmini,"alisema.

Alisema lazima ifike hatua wao kama serikali kuja na maelezo yanayofaa, ili kama kuacha ama kuiboresha gongo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470 DODOMA,**
**02.05.2022**

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.05.2022 hadi 17.05.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi,** gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

216843002

# Majaliwa atoa uamuzi mgumu MSD

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amefanya ziara katika Bohari ya Dawa (MSD) na kuagiza watu wote waliohusishwa na tuhuma za ubadhirifu zilizoainishwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wachukuliwe hatua.

Majaliwa amesema hoja zote zilizotolewa katika ripoti ya CAG lazima zifanyiwe kazi na tayari Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) imeanza kufanyia kazi hoja zote zilizotolewa kuhusu MSD.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi na watendaji wa MSD baada ya kutembelea viwanda vya kutengeneza barakoa na dawa vilivyoko katika eneo la MSD, Keko jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia kuhusu baadhi ya hoja za CAG, Waziri Mkuu alisema MSD ilifanya ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni tisa (9) bila ya mikataba halali jambo ambalo si sahihi.

Pia Waziri Mkuu amesema taasisi hiyo ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.52 kwa wazabuni sita (6) bila ya kufuata utaratibu na wala kuitaarifu Bodi ya Zabuni ya MSD.

Alisema MSD ilifanya zabuni 23 zenye thamani ya shilingi bilioni 8.55 zilifanywa nje ya Mfumo wa Ununuzi wa TANeps unaosimamiwa na PPRA kinyume na matakwa ya sheria ya ununuzi.

"MSD ilifanya malipo ya awali kiasi cha shilingi bilioni 14.89 kwa wazabuni watano (5) bila ya mikataba yoyote au makubaliano mengine ambayo yanabainisha msingi wa malipo ya awali."

Amewataja wazabuni hao kuwa ni Keko Pharmaceutical Industry; Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini; Nakuroi Investment Company Ltd.; Technical Services and General na Wide Spectrum (T) Ltd.

Alisema taasisi hiyo iliendesha mchakato wa ununuzi na kutoa mkataba wa kusambaza "Liquid Syrup" wenye thamani ya shilingi milioni 898 bila ya kushirikisha Bodi ya Zabuni ya MSD.

Alisema taasisi hiyo ilitumia kiasi cha shilingi milioni 215 kwa ajili ya kugharamia posho ya watumishi watatu waliokwenda China kwenye majadiliano ya kuleta mashine za dialysis kwa siku 61.

"Watumishi watatu wameenda China kufanya majadiliano kwa nini wasimtumie Balozi wa Tanzania nchini China kufanya shughuli hiyo. Si utaratibu kukaa siku 61 kwa ajili ya majadiliano tena bila ya kuhusisha menejimenti ya taasisi."

Majaliwa amesema katika taasisi hiyo kuna udhahifu wa usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi licha ya kuwa wamelipwa. "Lazima mjipange vizuri katika utendaji kazi wenu."

Amesema katika idara ya manunuzi kumebainika kuwapo kwa watumishi ambao si wataalamu, hivyo ameagiza wote 16 ambao si wataalamu waondolewe na kuwekwa watumishi wenye taaluma hiyo.

Mheshimiwa Majaliwa amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa MSD, Mavere Tukai, afanye tathmini ya utendaji ndani ya MSD na achukue hatua pale atakapobaini kuwepo na dosari. "Ni muhimu kuimarisha eneo la ufuatiliaji."



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akizungumza katika kikao cha tathmini ya kazi inayoendelea kufanywa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) hapa nchini kuhusu hali ya uchumi na kisera, jijini Dodoma. Kushoto ni kiongozi wa timu hiyo ambaye ni mshauri wa masuala ya uchumi na fedha wa (IMF), Idara ya Afrika, Charambos Tsangarides na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba. **Habari ukurasa wa 3.** **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Mgombea TLS aja na vipaumbele 10

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa Chama cha Mawakili wa Serikali (TLS), Prof. Edward Hoseah, ameweka bayana mambo 10 aliyoyasimamia kwa kipindi cha mwaka mmoja na atakayoyakamilisha katika kujenga chama imara na endelevu akipewa nafasi nyingine.

Akizungumza na waandishi wa habara jana kuhusu nia yake ya kutetea nafasi hiyo kwa mwaka mwingine, alisema aliyoyafanya yameacha alama na kubadilisha maisha ya mawakili na kwamba akipewa nafasi nyingine atakamilisha mengi zaidi.

Wagombea wengine kwenye nafasi hiyo ni Wakili Harold Sungusua na Jeremia Mtobesya.

Cha kwanza ni kuhakikisha TLS inawekeza ili kuondokana na kutegemea wanachama ambao michango yao ni Sh. milioni 600, huku mahitaji ya kuendesha chama hicho ni Sh. bilioni 6.

"Kutegemea michango ya wanachama pekee kuendesha chama ni ngumu sana, TLS hatuwezi kujidanganya kuwa inawezekana ndiyo maana nataka tuwekeze ili tuwe na vitega uchumi vya kutuingizia fedha tuache kusumbua wanachama,"alisema.

Cha pili, TLS imefanikiwa kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo (SACCOS), ambayo imeshakamilisha taratibu zote na hivi karibuni watakabidhiwa cheti cha usajili na kuanza kazi baada ya kuchagua uongozi, na kwamba kitahudumia wanachama wake nchi zima kuondokana na hali ngumu ya kiuchumi.

Tatu, alisema kwa kipindi cha mwaka mmoja wameimarisha utoaji msaada wa kisheria kwa wananchi na kuona mahitaji ni makubwa kiasi gani na kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria watafungua ofisi za kudumu.

"Tunataka msaada wa kisheria uwe endelevu, kwa sasa tunafanya kwa wiki moja ambayo bado haitoshi, nikipewa nafasi ya kuongoza tutafungua dirisha maalum la msaada wa kisheria ili tuwafikie wengi zaidi,"alisema.

Nne, alisema ikiwa atapewa nafasi hiyo tena ataimarisha taasisi ya kitaaluma ya kuwajengea uwezo wanasheria (Professional Enhancement Institute), itakayoongeza weledi kwa mawakili ili washindane kimataifa.

"Tunataka mawakili wetu wakienda Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na kwingine waweze kushindana na kufanya vizuri zaidi, hilo litawezekana kwa uwepo wa taasisi hii ambayo itawanoa zaidi," alisema.

Tano, kuhusisha serikali kwenye mambo mbalimbali yenye kujenga, ambayo yameleta manufaa makubwa kwa kuwa wamefanyakazi kwa karibu na kutatua changamoto nyingi ambazo zilishindikana.

"Tumewekeza zaidi kwenye hoja za kijenga na kutatua migogoro badala ya kuja na hoja hasi, migogoro mingi imetatuliwa bila kutumia lugha ngumu au kuumizana na ndiyo maana mambo yetu mengi yamekubaliwa na serikali," alifafanua.

Sita, kujenga kituo cha kimataifa cha upatanisho (Tanzania International Arbitration Center), ambacho kitatumiwa na wawekezaji waliopo nchini, ili kuondoa ulazima wa kwenda kufungua kesi nje ya nchi.

"Tunataka kituo hiki kiwe cha kimataifa kitumiwe na kila mtu aone Tanzania ni pa kukimbilia, tunashukuru serikali imekubali kutoa fedha za ujenzi wa kituo hiki, haya yote yamewezekana kwa kuwa tumekuwa na mazungumzo ya kuhusisha serikali zaidi kuliko kugombana," alisema Prof. Hoseah.

Saba, kwa mujibu wa Prof. Hoseah kutokana na kuihusisha serikali inajivunia kwa kipindi cha uongozi wake TLS itapata zaidi ya Sh. milioni 450 ambazo zilipaswa kurudishwa baada ya serikali kukusanya kwa mawakili.

Nane, kuhakikisha mawakili wanapata bima ya afya, na kwamba waliwawekeza mazingira mazuri kwa gharama kushuka kutoka Sh. milioni moja hadi 500,000.

Tisa, Prof. Hoseah alisema ndani ya mwaka mmoja wamefanikiwa kuwa na kiwanja jijini Mbeya chenye ukubwa wa ekari 10, na kwamba wameanza mkakati wa kuwekeza ili kuondokana na utegemezi wa ada za wanachama pekee.

Kumi, alisema kusaidia mawakili vijana ambao wameanza kazi wakati ambao kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha, na kwamba kwa mazungumzo na serikali zuio la mawakili wa kujitegemea kusimamia kesi za serikali na taasisi zake limeondolewa na baada ya taratibu kukamilika watarudi kama zamani, hali ambayo itaondoa ukata unaowakabili.

Pia, Prof. Hoseah alisema chini ya uongozi wake wamesimamia maadili ya mawakili, pamoja na kutoa msada kwa waliopata changamoto kutokana na kazi zao.

# TCRA yataja sababu kupanda bei kifurushi

Na Mary Geoffrey

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema kwa sasa gharama za kuuza data nchini ni kati ya Sh. 2.03 kwa MB moja hadi Sh. 9.35 kwa MB moja.

Aidha, imetaja sababu za kuongezeka kwa vifurushi hivyo kuwa gharama za uendeshaji wa vifaa vya mitandao ya mawasiliano vinavyotengenezwa na kampuni chache duniani.

Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta TCRA, Dk. Emmanuel Manasseh, aliyasema hayo katika mkutano wake wa waandishi wa habari kuhusu gharama za data.

Alisema gharama halisi ya mtoa huduma kuuza data na kurudisha gharama zake za uendeshaji ni Sh. 9.35 kwa MB moja na kutoa huduma zenye ubora na kuwafikia wananchi wengi.

"Kwa mujibu wa utafiti mbalimbali wa bei za huduma za data, nchi yetu kwa sasa ndio ina bei ya chini zaidi ya MB kwa nchi za Afrika Mashariki na SADC na wastani wa gharama za data nchini ni takribani Dola za Kimarekani 0.75 kwa GB moja ya data sawa na Sh. ya Tanzania 1.725 ambayo ni sawa na MB 1.68," alifafanua.

Alieleza sababu nyingine za kupanda gharama za data ni uwekezaji mkubwa unahitajika ili nchi nzima ipate mawasiliano bila kujali uchumi na idadi ya watu wake.

Alisema pia teknolojia zinabadilika kila mara na hivyo kuongeza gharama za uwekezaji.

Alitaja sababu ya bando kumalizika haraka ni kuongezeka kwa uwezo wa kupakua kutoka 3G hadi 4G kuongeza kutoka MB tatu kwa sekunde hadi MB 10 kwa sekunde moja bando linakatika kwa haraka.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Jabir Bakari, alisema TCRA wana jukumu la kusimamia bei za huduma za mawasiliano ikiwamo miundombinu, gharama za uwekezaji na uendeshaji.

Alisema vifurushi vilivyoko sokoni ni sahihi na kwamba vipo vinavyopanda, vipo vinavyushuka na vipo vilivyobaki vilevile.

Alisema sheria inawataka watoa huduma watoe tangazo kwa watumiaji wa huduma kupitia magazeti na vyombo vyao.

"Serikali inafanyia kazi baadhi ya gharama za uendeshaji kwa watoa huduma ili kutoa unafuu kwa watumiaji wa huduma pamoja na kusimamia matangazo ya kupanda kwa kifurushi kuwafikia wananchi," alisema Bakari.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika kikao cha wadau wa NGOs cha kutoa maoni ya kuandaa mkakati wa kuwezesha mashirika yasiyo ya kiserikali kuwa endelevu na kuwataka wadau hao kutumia kamati yao kutoa maoni ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Royal Tour yaleta fursa biashara hewa ukaa

Na Maulid Mmbaga

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema moja ya faida za filamu ya 'Royal Tour' ni kuanza kuuza hewa ya ukaa huku akibainisha kuwa tayari wadau mbalimbali duniani wamejitokeza kuja kutathmini misitu nchini kwa ajili ya biashara hiyo.

Akihutubia wakati wa hitimisho la uzinduzi wa filamu hiyo uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam, alibainisha kwamba amefanya mazungumzo pia na wadau wakubwa wa utalii na wako tayari kuja nchini.

"Nimefanya mikutano kadhaa na 'giant' wadau wakubwa wa sekta ya utalii ii nao pia baada ya kuona hii filamu, wameahidi kuja lakini filamu hii imeonyesha hali ya mazingira na misitu ya Tanzania, tayari tushapokea maombi ya watu wa hewa ukaa kuja kufanya tathmini ya msitu wote waliouona ili tuanze kuvuna fedha za hewa ukaa," alisema Rais Samia.

Kwa upande wake Kamishna wa Uhifadhi Prof. Dos Silayo, alimshukuru Rais kwa kuionyesha na kuizungumzia vizuri misitu kupitia filamu hiyo kiasi cha kuwavutia wawekezaji wengi kuja nchini kuwekeza hususani katika biashara ya hewa ukaa.

Alisema wadau hao wameamua kushirikiana na Tanzania ili kuweza kuimarisha misitu ili iweze kuwa sehemu ya chujio la hewa chafu duniani na kupunguza mrundikano wa gesi joto inayosababisha kuongezeka kwa joto duniani.

"Eneo la biashara ya hewa ukaa limeonekana kuwavutia wawekezaji wakubwa duniani katika bara la Asia na Marekani kuja kuwekeza na tayari kuna wawekezaji waliojitokeza tuko kwenye mazungumzo nao," alisema Prof. Silayo.

Aidha, alieleza kuwa Wakala wa Huduma za Misitu nchini umejipanga katika maeneo matatu ikiwamo kuhakikisha uhifadhi wa misitu unakuwa imara, maeneo ya vitutio vya misitu kutumika kuvutia wawekezaji kwenye suala la utalii na kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji katika viwanda vya misitu na nyuki.

Alisema kazi kubwa iliyofanywa na Rais itasaidia wangu wengi kuifahamu Tanzania na kuona umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya misitu hususani kilimo cha misitu na upandaji wa miti itakayosaidia uoto asili kubaki katika hali ya usalama.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Center ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 20th June 2022. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20th May 2022

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV

Maombi yatumwe kwa:

**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543, Dar**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 ,**
**Landline: +255222842543**

**ATCL TRAINING INSTITUTE.**




**Welcomes you, to where you can Fly**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Serikali iwapunguzie usumbufu na gharama waombaji wa ajira

**KWA** takribani miaka mitatu kila inapotangazwa nafasi za kazi za utumishi wa umma watu hujitokeza kuomba na ambao waliopita hatua ya awali ya mchujo hutakiwa kwenda kufanya usaili kwenye vituo walivyoelekezwa.

Mathalani, Idara ya Uhamiaji ilitangaza nafasi za kazi wakajitokeza waombaji zaidi ya 10,000 iliwalazimu kufanyia usaili uwanja wa taifa.

Aidha, Desemba mwaka 2021 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ilitangaza jumla ya watu 22,106 waliitwa kwenye usahili wa nafasi za ofisa uchunguzi na maofisa uchunguzi wasaidizi wakiwania nafasi 350.

Wote walitakiwa kwenda Dodoma kwa ajili ya usaili wa maandishi ambao ulifanyika kwenye vyuo vitatu tofauti, huku vingine vikiwa nje ya mji ambako wahusika wanapaswa kutumia gharana.

Hivi karibuni, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitangaza nafasi za ualimu na afya ambazo zinataka watu zaidi ya 12,000.

Tathmini ya maombi iliyotolewa na wizara hiyo ilionyesha kuwa kuna waombaji zaidi ya 83,000 ikiwa ni wastani wa waombaji zaidi ya 16,000 kwa siku, jambo linaloonyesha hali ngumu ya ajira iliyopo nchini kwa sasa.

Kilichotusukuma kuandika tahariri hii leo ni namna wanaoomba nafasi hizi wanaitwa kwenye usaili inakuwa ni ya kuwagharimu sana wao na familia zao, ili hali hawana kazi wala kipato.

Unapowasafirisha waombaji hawa kutoka mikoa mbalimbali ambao wengine wanasafiri zaidi ya saa 12, wanakwenda Dodoma ambako wanatakiwa kupangisha hoteli, lodge au nyumba za kulala wageni kwa siku tatu au nne watakazokuwa hapo ni kuwaumiza.

Mathalani, mtu anayetoka Kasulu, Kigoma au Sumbawaga au eneo jingine la pembezoni kabisa ambaye familia yake imeshamsomesha hadi chuo kikuu sasa inataka kuona akitoa msaada kwa familia, naye anatakiwa asiwe na chini ya shilingi 200,000 kwa ajili ya usaili ambao hana uhakika wa kupata ajira kutokana na ushindani.

Anapotakiwa kusafiri atatakiwa kuwa na nauli, chakula na mahitaji mengine, jambo ambalo ni gumu kwa watu maskini ambao ndiyo wanatafuta kazi ili kujikwamua.

Tunadhani lazima serikali iliangalie hili kwamba mchakato wa usaili ufanyike kwa njia ya mtandao kupunguza idadi ya wanaovuka hatua ya pili ya mchakato huo. Aidha, kama inawezekana muhimu usaili ukafanyika kwa kanda za nchi ili kuwapunguzia wahusika gharama, hata serikali yenyewe kutumia gharama kubwa kuwaweka maofisa kwenye mchakato huo kwa muda mrefu na kuwagharamia. Kwa mfano, waombaji kutoka Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam na Tanga wanaweza kupangiwa kanda yao. Arusha, Kilimanjaro na Manyara eneo moja pia.


Mikoa ya Kanda ya Ziwa kama Kagera, Shinyanga, Mara, Mwanza, Simiyu na Geita wanaweza pia kuwa na kituo chao. Hivyo hivyo, mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida inaweza kuwa na kituo kimoja wakati Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa pia inaweza kuwa na kituo kimoja. Kadhalika, mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma inaweza kuwakutanisha pamoja waombaji kutoka maeneo hayo wakati mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe inaweza kuwa na kituo kimoja.

Kwa kutumia utaratibu huu, serikali itawapunguzia mzigo wa gharama, usumbufu na mateso waombaji wa nafasi za ajira ambao wengi ni kutoka familia maskini. Tunawashauri wabunge wetu kuliona hili na kulipigia kelele katika mkutano unaoendelea hususan wakati wa makadirio ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora).

Kuwasafirisha watu zaidi ya 83,000 kwenda Dodoma na wakati huo huo kuna shughuli nyingine zinaendelea kama za mikutano ni kuwatesa kwa kuwa watahangaika kupata mahali pa kulala, kwa kuwa Jiji la Dodoma bado halijaweza kujitosheleza kwa wageni wote kwa wakati mmoja.

Ni muhimu kuangalia jambo hili ili kupunguza usumbufu na kupoteza muda, kwa sasa dunia imepiga hatua kutokana na ukuaji wa teknolojia, umerahisisha utendaji kazi wa kila siku, hata usaili unaweza kufanyika kwa njia ya mtandao katika kuchuja kundi la awali na kubali na wachache wa kusonga mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Wanawake watumie TEHAMA kupinga ukatili kijinsia

**JUMAPILI** Mei 8, ilikuwa siku tulivu kwa wanawake ambayo imepewa jina la Siku ya Mama –Mama's day. Ilikuwa ni wasaa mwingine wa kuwapa kinamama mahaba, pongezi, kuwazawadia, kuwashika mikono na kufurahi pamoja nao kutokana na kazi kubwa wanazozifanya kwenye jamii kama kuzalisha vyakula mashambani, kujenga uchumi wa taifa na wa familia na kutunza jamaa kuanzia watoto, wazee na wagonjwa.

Wakati kinamama wakifurahia, kujirusha na kufurahi pamoja na jamaa zao, ukweli ni kwamba wanahitaji kuwapo na juhudi zaidi kuwaondoa kwenye madhila mbalimbali yanayowazonga kama kutengwa kiuchumi kutokana na mifumo ya utoaji mikopo kuendeleza ubaguzi.

Siku ya Mama inapoadhimishwa baadhi ya taasisi za fedha zinapenda kuona matajiri wakikopa lakini si kinamama ambao huchukuliwa kuwa hawana cha kuweka reheni. Au ni vigumu kupata fedha na kurejesha mkopo wakiamini kuwa kipato na biashara zao si kubwa. Hata hivyo kinamama wa Tanzania wanaifurahia hatua ya kuwa sehemu ya wanufaika wa mikopo ya serikali wanayoipata kupitia halmashauri zao.

Changamoto nyingine inayowabana ni ushiriki mdogo katika masuala ya kisiasa na ya umma na hili linasababisha juhudi za kufikia uongozi wa usawa wa kijinsia wa 50/50 kwenye ngazi za uwakilishi, ujumbe kwenye mabaraza na kamati mbalimbali kuwa mdogo.

Si hivyo tu hata kwenye masuala ya uteuzi na uongozi wa kisiasa kama mawaziri, majaji, wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa taasisi za umma na binafsi, wakuu wa vyuo na wajumbe wa bodi na hata mabalozi kuendelea kuwa na idadi ndogo ya wanawake ikilinganishwa na wanaume.

Kinamama wengi kutokuwa na fursa za elimu kunakochangiwa na wasichana kushindwa kubakia shuleni kuanzia darasa la kwanza hadi vyuo vikuu, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba za ututoni, mila za kukataa kusomesha wasichana, umaskini kwenye familia na pia changamoto za maumbile kama kukosa jinsi ya kujisitiri wakati wa hedhi.

Masuala ya ukatili wa kijinsia na udhalimu dhidi ya wanawake yanaendelea kuanzia wanawake kutelekezwa na watoto, wanaume kukataa wajibu wa kutunza familia na kupenda kulelewa badala ya kulea, wanawake kuuawa na wenza wao kwa madai ya wivu wa mapenzi, kunyang'anywa mali na kudhulumiwa ndani ya familia zao.

Tatizo jingine ni kuwapo na utamaduni wenye madhara unaokumbatia mila za ukeketaji, kudharau hali ya ujauzito, wengine wakisema mimba si ugonjwa hata ng'ombe anazaa na kuwatumikisha wajawazito hali inayowaumiza kiafya pamoja watoto wao. Kuna unyago unaowafunza mafunzo ya kingono mabinti, vijijini na ngoma zisizo na maadili kama vigodoro.

Changamoto nyingine inayowatesa kinamama ni kutengwa kwa wanawake kwenye meza za mazungumzo iwe ni migogoro ya ardhi, mifugo, matatizo ya kukosekana amani kama ujambazi mitaani yote hayo yanazidi kuwaweka pembeni na kuwa watumwa wa unyanyasaji kijinsia, mathalani mahali pa kazi na mitaani.

Wakati Siku ya Mama ikiadhimishwa, dunia inatawaliwa na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) hivyo ni wakati wa kupiga simu, kutuma ujumbe wa SMS, kutumia whatsap na twitter kueleza kila kiovu kinachofanywa dhidi yao.

Kutumia TEHAMA kuuhabarisha umma kunaweza kupunguza ukatili, unyanyasaji na dhuluma kwa wanawake na kuongeza ushiriki wao katika uchumi, siasa na masuala ya kijamii kwa kupambana na wale wanaokwamisha.

Wanawake watumie teknolojia kueleza kila uovu wanaofanyiwa kuwa kwamisha kwa sababu woga wao ndiyo ni mauti yao, teknolojia itumike hata kueleza habari za wanaume wanaowakwaruza viganja wakati wa kusalimiana.

Yote hayo yataondoa hisia za unyanyasaji wa kijinsia kuwa ni jambo la kawaida na kuwalazimisha kulikubali na kulitarajia.

HABARI KITAIFA

# Mkakati wa kupunguza uagizaji mafuta ya kula, sukari watajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja bungeni mkakati wa kuondokana na uagizaji wa sukari na mafuta ya kula nje ya nchi ndani ya miaka mitatu ijayo ikiwamo kuongeza uzalishaji kupitia kwa wakulima wadogo na kutoa nafuu ya kikodi kwa wawekezaji wakubwa.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wabunge wakati akihitimisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2022/23.

Alisema Tanzania itajitosheleza kwa sukari na mafuta ya kula ifikapo mwaka 2025.

"Ni kweli kwamba Tanzania haijitoshelezi kwa sukari na mafuta ya kula na kuwa upandaji wa bei ya mafuta ya kula inasababishwa na mambo yaliyo ndani na nje ya uwezo wa nchi," alisema.

Alieleza kuwa Tanzania inatumia mafuta ya kula tani laki sita kwa mwaka wakati uwezo wa nchi wa uzalishaji ni wastani wa tani 250,000 hadi tani 300,000 na asilimia 70 ya mafuta yanayozalishwa ndani ya nchi yanatokana na zao la alizeti.

"Takwimu zinaonyesha kuwa upungufu sukari ni tani 100,000 kwa mwaka, linapotolea tatizo duniani kama lilivyo Covid-19 na vita kati ya Urusi na Ukraine, upande mmoja ni balaa na upande mwingine ni fundisho kwa sisi Watanzania, kwani hapa tulipo ni maamuzi tuliyoyafanya miaka ya 90 kwa kuamua kutolinda viwanda na sekta binafasi na sheria zingine zilipita ndani ya Bunge," alisema.

Aliongeza "Leo tunajadili ni kwa nini hatuna mafuta, hatuna viwanda, lakini tulikuwa na kiwanda cha mbolea, kama nchi tumeamua kutubu na kurudi kwenye misingi na kuwajibika kama nchi, isiwe kuinyoshea kidole serikali, serikali ilitekeleza maamuzi yaliyopitishwa na bunge hili na sheria zilipitishwa humu humu na tulikwenda kwenye mfumo wa uholela tukaua mambo yetu ya msingi kama nchi."



Alisema Serikali ya awamu ya sita inachukua hatua za kisera ambazo zitatekelezwa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango na imeanza kulinda viwanda vyake vya msingi na kuwa ifikapo mwaka 2025, nchi itajitosheleza kwa sukari na mafuta ya kula.

"Wizara kupitia TIRDO (Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda) tunakwenda kuimarisha viwanda vidogo vigodo vya sukari ambavyo vitakuwa vikizalisha tani 24 za sukari kwa mwezi," alisema.

Kuhusu mafuta ya kula, Bashe alisema mwaka huu, wizara imefanya majaribio kwa kugawa mbegu za ruzuku za alizeti tani 3,000 katika mikoa mitatu na kuwa msimu ujao itagawa tani 5,000.

Pia alisema wanachukua hatua za kikodi kulinda viwanda vya ndani ili vizalishe mafuta ya alizeti.

"Hatutamaliza tatizo la mafuta kwa mwaka mmoja ila kwa uwezo wa Mungu ndani ya miaka mitatu tutajitosheleza kwa mafuta. Hatua ya pili ambayo ni ya muda mrefu ni kuimarisha kilimo cha michikichi kwa kuwashirikisha wakulima wakubwa,"alisema.

Alisema serikali imetoa hekta 10,000 eneo la Rufiji kwa Bakhresa kwa ajili ya kilimo cha michikichi na pembeni yake kutakuwa na wakulima wadogo ambao watauza mazao yao kwa mwekezaji huyo atakayehusika kuyakamua.

"Serikali inakwenda kujenga viwanda vidogo Kigoma Manipaa vya kukamua mafuta," alisema.

Pia alisema ni lazima kukubali kama nchi kuanza kutoa ruzuku maeneo ya msingi.

"Serikali inachukua hatua ya kupunguza gharama za riba, hatua za kikodi kuanzia mwaka ujao wa fedha, gharama za kikodi kwa ajili ya kulinda viwanda muhimu, kutoa ruzuku kwa mazao ya mafuta na mbolea iwe jua ije mvua," alisema.

Miongoni mwa wabunge waliochangia eneo hilo ni Mbunge wa Mufindi Mjini(CCM), Cosato Chumi, alisema kwa miaka 10 amekuwa akizungumzia suala la sukari na mafuta ya kula na kwamba kama taifa kuna mambo yanahitaji yakataliwe.

"Inatakiwa kufika mahali kuna mambo tuyakatae, kati ya mambo tunayotakiwa kukataa ni kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo tunazalisha hapa nchini, haiwezekani tuagize ngano, sukari, mafuta ya kula,"alisema.

Alisema mfumuko wa bei na ugumu wa maisha uliopo unatokana na kila kitu kuagizwa nje ya nchi. "Kitu ambacho hatuagizi ni hewa tu, mimi nashauri tukatae kama taifa, tutakataaje? Mwaka 2019 niliandika barua pamoja na mchango wangu wa maandishi kwa Mawaziri wa Viwanda na Biashara, Kilimo, TAMISEMI na Fedha niliandika kueleza namna tutakavyoondokana na uagizaji sukari kila mwaka."

Alisema Brazil na India wamefanikiwa kwenye suala la sukari kwa kutumia viwanda vidogo kwenye maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo cha miwa na gharama zake sio kubwa katika kuwekeza.

"Kwanini nashauri tuwekeze huko kwasababu kiwanda hakihitaji heka tano tu na pia unahitaji heka kama 3000 za kuzalisha miwa, ndio maana niliwaandikia watu wa kilimo, TAMISEMI unaweza kushirikiana na Halmashauri, Wizara ya Fedha ikatoa fedha na uwekezaji wake hauwezi kuzidi dola za Marekani milioni 3.5 hadi 5, unazungumzia shilingi bilioni 8.

Alisema kuwa maeneo yapo kutokana na nchi ina maeneo tofauti tofauti na kushauri Wizara ya Viwanda kuunda kikosi kazi kwa ajili ya uchumi na kukataa mambo ya kuagiza bidhaa nje ya nchi.

## Wazalishaji kuku walia bei sokoni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa kiwanda cha Animal Care kilichoko Mlandizi Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Dk. Salaa Hamdun ameiomba serikali kusaidia kudhibiti bei ya kuku sokoni ili wafugaji wapate faida katika biashara hiyo.

Dk. Salaa alitoa ombi hilo jana baada ya Mwenge wa Uhuru kupita katika kiwanda chake na kukagua shughuli za uzalishaji zinazofanyika.

Alisema bei ya kuku sokoni bado ni ndogo ambayo inambana mkulima kwa kushindwa kupata faida ukilinganisha gharama za vyakula vya kuku hali ambayo wakati mwingine inasababisha baadhi yao kushindwa kuendelea na biashara.

"Serikali yetu ingeweza kutusaidia kwa wafugaji wetu, kusimamia masoko yao na kudhibiti bei mfano wanaouza kuku na maziwa bado bei ni ndogo ukilinganisha na gharama za vitu vingine kutokana na hali hiyo hata sisi tunaathirika moja kwa moja," alisema.

Alisema kwasasa wanakabiliana na kikwazo cha malighafi hususani zile wanazotoa nje ya nchi kama soya wanazotoa Zambia na Malawi, lakini wakati mwingine mahindi hasa pale yanaporuhusiwa kwenda nje inaawaathiri wawekezaji wa viwanda vya ndani.

Dk. Salaa alisema katika kiwanda hicho wanatengeneza fursa za moja kwa moja kwa wafugaji ambao wako katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kiwanda hicho ambacho kinazalisha vyakula vya mifugo na virutubisho kinatumia malighafi za mahindi, dagaa na alizeti kimejikita pia katika kutoa elimu ya ufugaji kwa vijana.

Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa wameweza kutoa ajira za moja kwa moja 200 na kwamba kitendo cha Mwenge wa Uhuru kufika katika kiwanda hicho wanaimani itazidi kufungua fursa mbalimbali.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahil Geraruma, amepongeza uwekezaji wa kiwanda hicho ambao unakwenda kupunguza tatizo la ajira.


## NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEMEKE | MWANNE HASSAN SULEIMAN | NYUMBA | MWANNE HASSAN SULEIMAN | MAMBOLEO-SANDALI TEMEKE | 25/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ALLY SAIDI MOHAMED | NYUMBA | ALLY SAIDI MOHAMED | MAJOHE KICHANGANI | 26/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | HAPPYNESS DANIEL RWEHUMBIZA | NYUMBA | DAUDI MUSA SUNTA | MBEZI MSUMI | 27/05/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba au Kiwanja ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0715363537**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216848502

# Waziri aonya matumizi silaha za maangamizi

Na Joseph Mwendapole

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana, amesema nchi za Afrika zinapaswa kufanya kila linalowezekana kuhakikisha silaha za kibaiolojia zinazotokana na virusi mbalimbali hazitumiki kama silaha za maangamizi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili ulioandaliwa na Chama cha Wabunge cha Kimataifa (PGA), ambao unakutanisha wabunge 22 kutoka mataifa 14.

Wabunge hao wanajadili masuala mbalimbali za usalama ikiwamo matumizi ya virusi mbalimbali kama silaha za maangamizi na wabunge hao wanatoka nchi za Togo, Liberia Siera Leoni, Gambia Somalia, South Sudan, Zimbabwe na Marekani.

“Wakati mwingine masuala ya kibaiolojia kwasababu virusi hivi watu wanaweza kuvitumia kama silaha za maangamizi ndiyo maana nchi hizi zimekuja hapa kujadiliana namna ya kuhakikisha usalama na kuzuia matumizi ya virusi kama silaha,” alisema.

Waziri Chana alisema suala la kupambana na matumizi ya virusi kama silaha na kujali afya za watu linapaswa kupewa kipaumbele na mataifa mbalimbali kama kweli zinataka kuweka dunia katika hali ya usalama na amani.

“ Ni muhimu sana kwamba nyinyi mmeona uzito wa suala hili na kuamua kulijadili kwa ukubwa huu wa mataifa 14 kuja pamoja hapa Tanzania na ndiyo sababu mimi naona maazimio yenu ya leo yatakuwa muhimu sana,” alisema.

Akizungumzia ugonjwa wa COVID-19, Chana alisema watalii wanaotembelea Tanzania walipungua kwa asilimia 59 kutoka watalii 1,527,230 mwaka 2019 hadi watalii 620,867 mwaka 2020 na mapato pia yalipungua kwa asilimia 72.5 kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 hadi Dola bilioni 0.715.

Alisema kupungua kwa mapato hayo kulisababisha madhara makubwa kwa uchumi, biashara na ajira za watu wengi zilipotea ingawa mwaka 2021 hali ya matumaini ilirejea kwenye sekta ya utalii.

Chana alisema idadi ya watalii waliotembelea Tanzania kwa mwaka 2021 waliongezeka kwa asilimia 48.6 kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 na kufikia watalii 922,692 mwaka 2021.

Alisema mapato nayo yaliongezeka kwa asilimia 76 kutoka Dola za Marekani 0.715 bilioni mwaka 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021.

Mwenyekiti wa chama hicho nchini ambaye ni Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza, alisema Tanzania ilisaini mkataba wa kupinga silaha za maangamizi mwaka 1971 lakini haikuwa imeuridhia.

“Chama hiki kina ajenda nyingi kama Tanzania kujiunga na mkataba wa kupinga silaha za maangamizi, sisi tulisaini lakini hatukujiunga tulijiunga na mkataba huo mwaka 2015 baada ya mimi kujiunga na chama hiki,” alisema.

Alisema wabunge hao kutoka nchi 14 watakuwa na mjadala wa siku mbili kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo ndoa za utotoni na usalama wa silaha za kibaiolojia na watatoa maazimio.




Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi anayesimamia Uhifadhi na Maendeleo ya Biashara wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Bakari Mnaya, akizungumza katika uzinduzi wa aina mpya ya utalii wa baiskeli katika Hifadhi ya Arusha uliozinduliwa juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Serikali yatoa ushauri kwa mashirika yasiyo ya kiserikali

Na Sabato Kasika

WADAU wa mashirika yasiyo ya kiserikali wametakiwa kutumia kamati yao waliounda kutoa maoni yao ambayo yatasaidia kuwa na mkakati utakaoyawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kuyafanya yawe endelevu.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akifungua kikao cha wadau hao wa Kanda ya Mashariki, jijini Dar es Salaam jana.

Alifafanua kuwa Septemba mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza wizara hiyo kuandaa mpango mkakati wa kuyajengea uwezo mashirika yasiyo ya kiserikali ili kupunguza utegemezi na kuwa na uendelevu wa shughuli zao.

“Kwa kuzingatia umuhimu wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla, nitoe rai kwenu nyie washiriki wa mkutano huu kutoa maoni yenu yatakayosaidia kwa mkakati huu, siyo kwenda kusema pembeni au jukwaa ambalo silo,” alisema Dk. Gwajima.

Dk. Gwajima alisema, mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakichagiza jitihada za serikali kuwaletea wananchi wake maendeleo kupitia utekelezaji wa miradi ya afua mbalimbali ikiwamo ya afya, elimu, maji na mazingira.

“Lakini mchango huo upo pia katika miundombinu, utawala bora, nishati, ustawi wa jamii mifugo na uvuvi, uwezeshaji wa jamii na sekta nyingine mtambuka, ikiwamo kuboresha huduma za jamii na kuongeza fursa za ajira,” alisema. Alisema, wizara ilianza mchakato wa kuandaa mkakati huo Novemba mwaka jana na iliunda kamati ya wajumbe 20 ikijumuisha wataalamu kutoka wizarani, mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na wadau wengine,” alisema.

Waziri huyo alisema, hadi sasa kamati hiyo imefanikisha kukamilika kwa andiko la majadiliano, nyenzo za ukusanyaji wa taarifa na maoni kutoka kwa wadau mbalimbali.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Nesia Mahenge, alisema, imeshakusanya maoni kutoka katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo ni Mara, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Geita, kituo cha kukusanyia maoni kwa Mwanza.

Kikao cha leo ni kwa ajili ya maoni ya wadau wa kanda ya Mashariki ambayo inahusisha mikoa ya Dar es Salaam Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara, kisha tutakwenda Kanda ya Kaskazini,” alisema Nesia.

Aliongeza kuwa baada ya kutoka kanda hiyo ambapo kituo kitakuwa Arusha, watakwenda Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika kituo cha kukusanyia maoni ambacho kitakuwa jijini Mbeya.

“Baada ya kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, tutakwenda kanda ya kati ambapo kituo cha kukusanyia maoni ya wadau kitakuwa jijini Dodoma, hivyo wito wangu ni kwamba tuendelee kushirikiana ili tumalize kazi hii,” alisema.

## Dagaa kuwa zao la kimkakati Kigoma

Na Mbaraka Kambona, UVINZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wanatengeneza miundombinu mizuri na kuwapatia wavuvi wanaoishi kandokando ya ukanda wa Ziwa Tanganyika na maeneo mengine vifaa vya kisasa vya uvuvi ili viwasaidie kuongeza thamani ya zao la dagaa na kupunguza upotevu wa zao hilo baada ya kuvua.

Ulega aliyasema hayo wakati wa ziara yake aliyoifanya katika vijiji vya Buhingu na Katumbi vilivyoko wilayani Uvinza, mkoani Kigoma Mei 6 - 7, 2022.

Akizungumza na wavuvi wa vijiji hivyo kwa nyakati tofauti alisema Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kukuza uchumi wa buluu na ndio maana inatengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki ili kuwaongezea thamani na waweze kuuzika kwa bei nzuri na wananchi wafaidike na zao hilo.

“Tunataka tuone zao la dagaa ambalo huku Kigoma linazalishwa kwa wingi linainua maisha ya watu, hatutaki kuona hata dagaa mmoja anapotea kwa kuharibika au kuoza, lengo letu ni kuona ukanda wote huu wa Ziwa Tanganyika mnanufaika ipasavyo kupitia dagaa,” alisema.

Aliongeza kuwa wanawapatia wavuvi hao vifaa ikiwamo boti, injini, nyavu, kamba na taa lengo likiwa ni kufanya uvuvi endelevu na kulifanya zao la dagaa kuwa la kimkakati ili liwe chachu ya maendeleo kwa wavuvi hapa nchini.

“Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tunaendelea kutengeneza miundombinu mizuri ya kuchakata dagaa na mazao mengine ya samaki katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao hayo na kuyaongezea thamani ili yauzwe kwa bei nzuri ndani na nje ya nchi,” alifafanua.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Hanaf Msabaha, alisema kuwa kuna haja serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki wilayani humo ili samaki waweze kupatikana muda wote.

Mkurugenzi wa Mradi wa Tungane ambao unatekelezwa mkoani Kigoma, Lukindo Hiza alisema tayari wameshirikiana na uongozi wa Wilaya ya Uvinza kwa ajili ya kujenga mwalo wa kisasa utakaosaidia kupunguza upotevu wa dagaa na wataweza kuwaongezea thamani ili wawauze kwa bei nzuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

## Wanafunzi kuanza kupata masomo, mada mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kusaidia kurahisisha ujifunzaji kwa wanafunzi wa sekondari nchini, Taasisi ya Digital Academia (DATL) Tanzania imeanzisha programu ya mtandao ya TESEA App ambayo itamwezesha mwanafunzi kupata mosomo na mada mbalimbali kwa mujibu wa mtaala wa elimu.

Akizungumza katika uzinduzi huo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mvumbuzi wa TESEA App, Abdul Mombokaleo, alisema programu hiyo ni nyenzo tosha ambayo itamsaidia kujifunza kupitia simu ya mkononi (vishkwambi), tablet au kompyuta.

Wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita wataweza kupata mada za masomo kama Fizikia, Biolojia, Kemia, Hisabati na mengine mengi hivo kuongeza ari ya kujifunza.

"Kupitia programu ya TESEA APP wanafunzi wataweza kutafuta maudhui ya kozi, kununua usajili pamoja na kujifunza kupitia maudhui ya kozi ya video na sauti na kufanya majaribio ya kozi zilizokamilika na watahitajika kulipia kiasi cha 100/- tu kwa siku," alisema Mombokaleo.

Pia alisema wazazi kupitia simu zao au kompyuta wanaweza kufuatilia kwa karibu na kuchunguza kile ambacho kila mwanafunzi amekuwa akikifanya pindi atumiapo programu hiyo.

Akizungumzia namna ya kufungua programu hiyo Mombokaleo alisema baada ya kupakuliwa maudhui yanakuwa katika simu au kompyuta ya mtumiaji kila wakati kwa kuperuzi kwa urahisi na haraka.

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mameneja na Wamiliki wa Shule na Vyuo Visivyo vya Serikali Tanzania (TAMONGSCO), Dk. Alfred Luvanda, alisema programu hizo ni nyenzo ambazo zimekuwa zikihitajika zaidi kwani ziwawezesha wanafunzi kupata elimu bora na kwa uharaka zaidi.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwasaidia watoto kutumia programu hiyo kwani ni namna nyepesi ya kumsaidia kufikia malengo yake.

Katika hafla hiyo wanafunzi walipata fursa ya kushiriki katika mashindano ya chemsha bongo kama sehemu ya kuchochea utamaduni wa kujisomea na kujiendeleza kielimu na hivo kushindia tablets and pesa taslimu.

Constatine Swai, mmoja wa wanafunzi kutoka Sekondari ya Barabara ya Mwinyi wilayani Temeke, alisema programu hiyo itamsaidia katika masomo yake hasa katika kipindi cha likizo.

Swai aliibuka mshindi wa kwanza katika chemsha bongo na hivyo kuondoka na tablet mpya na pesa taslimu Sh. 200,000.

# Wawekezaji kutoka Czech waona fursa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza uwekezaji, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimewaalika wawekezaji kutoka Jamhuri ya Czech kuja kuwekeza nchini hasa katika sekta za kilimo, uvuvi na utalii.

Akizungumza baada ya kufanya mazungumzo na Balozi wa Jamhuri ya Czech nchini, Martin Klepetko, aliyeambatana na Balozi kutoka Idara ya Diplomasia ya Uchumi Wizara ya Mambo ya Nje ya Czech, Miloslav Machalek, Mkurugenzi Mtendaji TIC, Dk. Maduhu Kazi mbali ya kuwapatia taarifa mbalimbali za uwekezaji nchini, amesema Tanzania kwa sasa imekuwa sehemu maridhawa kutokana na uwepo wa rasilimali nyingi ambazo ni lulu kwa taifa.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa ujio wenu na hii inatupa picha sisi kama wadau namba moja wa uwekezaji nchini kuwa kuna kazi kubwa inafanywa na sio kwetu tu bali hata na Rais wetu ambaye amekuwa mstari wa mbele kuitangaza nchi," alisema Dk. Maduhu.

Dk. Maduhu aliongeza kuwa, kutoka Januari mpaka Machi mwaka huu, idadi ya wawekezaji 189 walikuja nchini kuangazia fursa zilizoko huku sehemu kubwa ya watu kutoka Jamhuri ya Czech wamevutiwa zaidi kuwekeza kwenye sekta ya utalii.

Balozi Martin Klepetko alisema Tanzania ni nchi yenye fursa nyingi ambazo zikiendelezwa na kutumiwa vyema manufaa makubwa yatapatikana na kusisitiza kuwa sekta ya uwekezaji ni sekta nyeti yenye kutengeneza ajira nyingi duniani.

"Ni faraja kubwa kwetu sisi kuwa hapa, tumejifunza mengi kupitia mazungumzo yetu, sekta hii ya uwekezaji ni pana lakini niwahakikishie kuwa ni sekta ambayo kwa kiasi kikubwa inapunguza changamoto ya ajira ikisimamiwa vyema," alisema Klepetko.

Klepetko aliongeza: "Kupitia mazungumzo haya na sisi tutakuwa mabalozi wa kutangaza fursa adhimu zilizoko hapa ili watu wa Czech waje kuwekeza Tanzania." Miloslav Machalek alisema maendeleo ya uchumi wa taifa lolote duniani yanategemea uwekezaji huku akibainisha kuwa sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta inayowavuta wa Czech wengi zaidi kuja Tanzania.

"Unapozungumzia uwekezaji unagusa moja kwa moja uchumi kwa kuwa sekta hizi zina uhusiano mkubwa sana kwa maendeleo ya taifa," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi (kulia), akijadiliana jambo na viongozi, wawakilishi wa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Norway na Uingereza baada ya mkutano uliowaleta pamoja watendaji wa taasisi za serikali na ujumbe wa wawekezaji na wafanyabiashara 37 kutoka nchini za Norway na Uingereza ulioratibiwa na Norwegian-African Business Association na Kampuni ya Invest Africa kwa kushirikiana na TIC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo akoshwa na Red Cross kwa kusaidia kukabiliana na majanga

**Na Yasmine Protace**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amekipongeza Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross Tanzania) kwa kufanyakazi kwa kujitolea katika kukabiliana na matukio ya majanga.

Jafo aliipongeza Red Cross kwa moyo wa kujitolea kwa kuisaidia jamii inapokumbwa na majanga ikiwamo na kufanya zoezi la upandaji miti kitendo hicho kinaonyesha ni cha kizalendo.

amewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kujitolea katika huduma za kijamii ikiwamo na uokoaji pale majanga yanapotokea.

Mbali na kujitolea katika huduma za kijamii pia amewataka Watanzania kujenga utamaduni pia wa utunzani wa mazingira kwa kupanda miti.

Jafo akiyasema hayo juzi, jijini Dodoma katika kilele cha maadhimisho ya siku ya chama hicho.

Maadhimisho hayo ambayo kwa Tanzania REDCROSS inatimiza miaka 60 toka kuanzishwa kwake mwaka 1962 yameambatana na zoezi la upandaji miti katika Hospitali ya Rufani mkoa wa Dodoma.

"Ni muhimu kwa kila Mtanzania kuendelea kujitolea utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti ikiwamo na kujenga utamaduni wa kujitolea pale majanga yanapotokea," alisema.

Aliongeza kuwa ni muhimu kwa kila Mtanzania kwa kuendelea kulinda amani ya Tanzania kwani kuna baadhi ya mataifa hayawezi kufanya sherehe zozote za maandamano kutokana na machafuko.

Jafo aliipongeza Red Cross kwa moyo wa kujitolea kwa kuisaidia jamii inapokumbwa na majanga ikiwamo na kuipongeza kwa kufanya zoezi la upandaji miti na kwamba kitendo hicho kinaonyesha ni cha kizalendo.

Pia Jafo alizungumzia suala la sensa ya watu na makazi, ambayo itafanyika Agosti 23, mwaka huu, ambapo aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi ili serikali iweze kuweka bajeti sahihi kwa ajili ya maendeleo.

Dk. Asha Mohammed, mwakilishi wa Red Cross nchini Kenya akizungumza kuhusu kazi zinazofanywa na Red Cross, alisema kuwa shirika hilo limekuwa likifanya kazi za kijamii kwa kujitolea pale panapotokea majanga.

Condester Sichalwe kutoka Mombasa nchini Kenya, aliipongeza RedCross kwa kuendelea kutoa huduma kwa jamii huku akitoa wito kwa chama hicho kufika zaidi vijijini ili wananchi wajue majukumu muhimu yanayotolewa na chama hicho.

# FCC yatekeleza mpango mkakati wa kumlinda mlaji biashara mtandaoni

TUME ya Ushindani (FCC), inatekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26 wa kumlinda mlaji wa biashara mtandaoni.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Judith Kapinga. Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kupitia FCC wa kumlinda mlaji katika biashara mtandaoni.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema katika kuhakikisha biashara ya mtandaoni inalindwa FCC ina mpango mkakati wa kutekeleza jukumu la kumlinda mlaji.

Alisema mpango mkakati huo ni kupitia njia ya elimu kwa walaji kuhusu haki na wajibu wao na mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wakifanya biashara za mtandaoni ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa taarifa zilizotolewa kwenye mtandao kuwa ni sahihi.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge huyo alisema suala la kumlinda mlaji na biashara za mitandao haliwezi kusubiri mpango mkakati na madhara makubwa yanaendelea kwa wafanyabiashara na walaji.

"Serikali ni lini itaona umuhimu wa kufanya utaratibu wa haraka wa kuweka kanuni ili kumlinda mfanyabiashara na mlaji katika biashara ya mitandaoni?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kigahe, alikiri kuwapo na mkakati huo na kudai kwamba hauwezi kusubiriwa kumlinda mlaji kwa kuwa biashara mitandaoni inaendelea.

"Tunafanya marekebisho ya sheria ya ushindani namba nane ya mwaka 2003 ina jukumu la kumlinda mlaji tumeanza kuhamasisha biashara mtandaoni na tumefungua kupitia Shirika letu la Posta mambo mengi yanafanyika hatuwezi kusubiri mpango mkakati," alisema.



Mbunge wa Momba, Condester Sichwale, akionyesha chupa za pombe ndani ya ukumbi wa Bunge alipokuwa akichangia hoja ya hotuba ya makadirio na mapato ya mwaka 2022/2023 ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji bungeni jana. Alitetea pombe za kienyeji kupewa vibali na TBS ili kuuzwa ndani na nje ya nchi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kiwanda cha mionzi dawa kuanza Juni

SERIKALI imeliambia Bunge kuwa kiwanda cha kutengeneza mionzi dawa kinatarajiwa kuanza kufanya kazi Juni mwaka huu.

Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Mtambwe, Khalifa Mohamed Issa (ACT-Wazalendo).

Katika maswali yake, mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuangalia namna ya kupunguza gharama za uagizaji wa vifaa tiba kwa ugonjwa wa saratani.

"Pia magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa yakiongezeka kila wakati lakini asilimia 20 ya fedha zinagharamia magonjwa haya, je, sio wakati muafaka sasa wa serikali kuunda tume ya kushungulikia magonjwa haya kama ilivyo TACAIDS?" Alihoji.

Akijibu mawali hayo, Naibu Waziri Mollel alisema kiwanda hicho kitaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa takribani nchi tano za Afrika kuwa na kiwanda cha aina hiyo.

Hata hivyo, alisema si jambo jema kuanzisha tume ya kushughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kuwa fedha nyingi zitatumika kwa ajili ya utawala badala ya fedha hizo kwenda kuwahudumia watu.

Alisema kinachopaswa ni kutoa elimu na kuimarisha utoaji wa huduma za afya.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mikakati ya serikali katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

Mollel alisema kuwa mkakati wa serikali katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ni kutoa elimu kinga, kusomesha madaktari bobezi kwenye eneo hilo pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba vya teknolojia ya juu katika utambuzi na tiba ya magonjwa yasiyoambukiza.




**Habari zote na Augusta Njoji**

# Sababu serikali mfumo wa kuunda e-RCS

BUNGE limeelezwa kuwa serikali za pande mbili za Muungano ziliunda mfumo wa kielektroniki wa 'Electronic Revenue Collection System (e-RCS)' wenye uwezo wa kutambua miamala ya simu inayofanyika.

Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Jang'ombe (CCM), Ali Hassan Omar King.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua ni lini Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itasitisha kukusanya na kuzirudisha fedha za Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) zilizokwisha kusanywa kutoka kwenye miamala ya mitandao iliyofanywa Zanzibar kwa kuwa kiasi kilichokusanywa ni asilimia 18, lakini fedha zilizowasilishwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ni asilimia 15 ya kiwango cha fedha ya makato hayo.

Akijibu swali hilo, Chande alisema Sheria za Kodi ya VAT kwa pande zote za Muungano zimeweka msingi wa kutoza na kukusanya VAT pale ambapo huduma inapotolewa.

Alisema huduma ikitolewa Tanzania Bara, TRA inatoza VAT ya asilimia 18 kwa mujibu wa sheria ya VAT inayotumika Tanzania Bara na huduma ikitolewa Zanzibar, ZRB inatoza VAT ya asilimia 15 kwa mujibu wa sheria ya VAT inayotumika Zanzibar.

"Ili kutambua sehemu ambapo huduma imetumika, serikali za pande mbili za Muungano ziliunda mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama 'Electronic Revenue Collection System (e-RCS)' wenye uwezo wa kutambua miamala yote inavyofanyika na hivyo kusaidia kutunza takwimu sahihi za mauzo yanayotokana na miamala ya mitandao inayofanywa na watumiaji wa kila upande," alisema.

Alisema mfumo huo unasimamiwa na kamati ya wataalamu wa kodi kutoka TRA na ZRB.

"Mifumo ya kampuni zote za simu hapa nchini imeunganishwa na mfumo wa Serikali wa e-RCS na taarifa za miamala ya mitandao hutolewa kila mwezi ikiainisha bayana huduma zilizotumika Tanzania Bara na zile zilizotumika Zanzibar," alisema.



Ukurasa 14

Wajasiriamali wawa mashujaa, kugeuza matatizo kuwa fursa



Ukurasa 12

Kujitokeza kuhesabiwa ni kufanikisha maendeleo yako



Ukurasa 13

## Ndivyo miji inavyotisha kiudhalilishaji kinamama

Nipashe

# TESA

Jumanne Mei 10, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU
NA GERALD KITABU

# Serikali, EU sasa kuwaonyesha Watanzania ulipo mlo wenye lishe

• Kujenga vituo vya misosi asilia Dar, Z'bar

SERIKALI na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) wamezindua kampeni ya kitaifa ya lishe inayolenga kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwajengea wananchi tabia zinazofaa za kula vyakula bora vinavyopatikana nchini.

Kampeni hiyo ya kitaifa italeta mambo mapya ikiwamo kuanzisha maeneo ya vyakula asilia ' msosi asilia' Dar es Salaam, Mbeya na Zanzibar ili kuimarisha mifumo ya chakula na lishe kwa kutumia vyakula vinavyopatikana katika maeneo watu wanayoishi.

Kampeni hiyo ya kitaifa inalenga kuwafikia Watanzania takribani milioni 32 inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia programu ya AGRI-CONNECT, inayowahimiza watu kushiriki kikamilifu.

Uzinduzi wa kampeni hiyo ambao pia ulifanyika pia Zanzibar, ulifanyika katika soko la Kisutu jijini Dar es Salaam ukianza na kuhamasisha, kutoa elimu na kupanua wigo wa mazingira bora na wezeshi ili Watanzania wabadili tabia na kuanza kula mlo wenye lishe unaopatikana sehemu wanazoishi.

Viongozi mbalimbali wa serikali na wadau wanasema inalenga kuimarisha lishe bora na kupunguza utapiamlo nchini, watu wakihimizwa kutumia vyakula vinavyopatikana kwenye mazingira yao.

Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Mkurugenzi wa Usalama wa Chakula katika wizara hiyo, Dk. Honest Kessy, anazindua kampeni hiyo akisema kipaumbele cha serikali ni kupunguza utapiamlo kwa kiwango kikubwa kadri inavyowezekana.



Wadau mbalimbali wakishiriki katika uzinduzi wa kampeni ya lishe bora: **PICHA: GERALD KITABU**

Anawaambia washiriki kuwa kampeni hiyo imekuja katika kipindi ambacho dunia inahangaika kukabiliana na kumaliza janga la UVIKO-19.

"Tumeimarisha usimamizi wa masuala ya chakula na lishe kwa kuhimiza uwekezaji zaidi katika kilimo, uzalishaji wa chakula na elimu ya lishe ili kuongeza upatikanaji na ufikiwaji wa milo iliyo bora kupitia uzalishaji katika kilimo na uelewa bora zaidi wa umuhimu wa milo bora katika kuzuia matatizo ya afya kwa sababu ya ukosefu wa lishe na kuimarisha kinga ya mwili," anasema Kessy na kuwataka wananchi kushiriki kikamilifu.

### YATAKAYOFANYIKA

Kauli mbiu ya programu hiyo ni lishe bora ni mtaji, kampeni hii ya kitaifa itajumuisha shughuli mbalimbali kama vile programu za mapishi, ziara za elimu ya lishe katika daladala, mafunzo kwa vijana wasichana na kuanzishwa kwa maeneo ya chakula au msosi asilia itakayoandaa vyakula vya Kitanzania Dar es Salaam, Mbeya na Zanzibar.

Ndani ya kipindi cha miaka miwili kampeni inatarajia kuwafikia watu milioni 32 kupitia majukwaa mbalimbali likiwamo la mitandaoni.

### TIJA YA PROGRAMU

Mwakilishi wa FAO nchini, Dk. Nyabenyi Tipo, anasistiza kwamba wakati janga la dunia likiendelea, umuhimu wa milo bora katika kukabili madhara yake ni wa muhimu zaidi.

Anaongeza kuwa mabadiliko katika tabia za jamii kuhusiana na uzalishaji wa chakula, ulaji, na ufikiwaji wa masoko utaongeza upatikanaji wa chakula, kuimarisha kinga ya mwili na kuwapa wakulima wadogo kipato.

Katika tukio hilo watu 100 wa kwanza kuwasili katika soko la Kisutu ulipofanyika uzinduzi huo walipewa kikapu cha chakula kilichojaa vyakula anuai vilivyoonyeshwa katika sahani ya mfano ya milo bora. Vyakula walivyopatiwa bure ni pamoja na nyama, samaki, mafuta, mbogamboga, matunda, viazi lishe, viazi mviringo, unga na maharage lishe.

Programu hiyo inayoongozwa na FAO inayoitwa kujenga uhimilivu wa mifumo ya kilimo na chakula na lishe bora katika muktadha wa janga la dunia ni nguzo ya nne ya mradi wa AGRI-CONNECT kusaidia minyororo ya thamani kuleta ustawi wa pamoja unaokazia zaidi lishe na kuanzisha mifumo ya kusaidia kupunguza makali ya janga katika upatikanaji wa chakula na masoko.

### UDUMAVU UNATISHA

Akizungumzia hali ya afya kwa watoto chini ya miaka mitano, mtaalamu wa lishe ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mafunzo na Elimu ya Lishe, Dk. Esther Nkuba, anasema asilimia 34 ya watoto wa umri huo nchini wamedumaa.

Anaongeza kuwa hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano ni kiashiria muhimu kwa afya ya mtoto.

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Kujitokeza kuhesabiwa ni kufanikisha maendeleo yako

AGOSTI 23, mwaka huu, itakuwa siku ya Sensa ya Watu na Mkazi ambayo Watanzania watahesabiwa ili kuijua idadi yao, kwa lengo la kufanikisa kuandaa na kupanga mipango ya maendeleo ya taifa kwa kuangalia vipaumbele, idadi ya watu na rasilimali zilizoko.

Siku hiyo ya sensa ilitangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwanzoni mwa mwezi uliopita, na sasa kinachoendelea ni serikali na taasisi mbalimbali zikiwamo za dini kuhimiza Watanzania kujiandaa kuhesabiwa.

Rais anawaagiza viongozi kutoa elimu na mafunzo kwa wananchi ili wajitokeze na kushiriki katika sensa, na kwamba ili ifanikiwe uelimishaji na uhamasishaji ni masuala ya kipaumbele na kwamba elimu inatakiwa kukabili changamoto za baadhi ya mila, desturi na imani potofu ndani ya jamii zinachukulia kuhesabiwa au kutaja idadi ya watoto au wanakaya kuwa ni kukaribisha mikosi na vifo.

Wakati Rais akihimiza hilo, Mufti wa Tanzania, Shekh Abubakar Zubeir, anawataka Waislamu kujitokeza kushiriki katika sensa hiyo, kwa kuwa ni jambo la wote na wasifuate kauli au yanayosemwa kuwa eti katika Uislamu hakuna sense.

Anawahimiza kutimiza wajibu wa kuhesabiwa wakati wa Swala ya Idd na kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki suala hilo kwa kuwa ni haki kwa Waislamu na Watanzania kujitokeza na kukubali kuhesabiwa kwa manufaa ya taifa.



Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, ofisi yake ndiyo inayosimamia sensa ya watu na makazi. **PICHA: MTANDAO**

### UMUHIMU WA SENSA

Mwenyekiti wa Kamati ya Sensa ya Watu na Makazi, ambaye ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa anasema, ndiyo itakayoiwezesha serikali kupata taarifa za msingi za kusaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025.

> Taarifa za kidemografia (umri wakati wa ndoa ya kwanza), maswali yanayohusu ulemavu (kichwa kikubwa na mgongo wazi, kifafa, mbalanga na usonji yataulizwa.

"Sensa inafanikisha kupata taarifa za mabadiliko na mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa, kwani taarifa za idadi ya watu huziwezesha mamlaka za wilaya kutekeleza mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi za chini na pia hutumia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali," Waziri Mkuu anasema.

"Lakini sensa inasaidia katika suala la kigawo katika kukokotoa viashiria vingine, mfano pato la mtu mmoja mmoja, la taifa, ajira na ukosefu wa ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi," anasema.

Anaongeza kuwa kupitia sensa, zinapatikana taarifa zitakazowezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira.

"Takwimu sahihi za sensa zinahitajika kwa ajili ya msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia, ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa," anasema.

### MASWALI YA SENSA

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, anataja maswali yatakayoulizwa wakati wa sensa kuwa ni taarifa za kidemografia kuanzia umri, jinsi, uhusiano, hali ya ndoa, uraia.

"Vilevile kutakuwa na maswali kuhusu ulemavu, taarifa za elimu uhamaji, pamoja na habari za Watanzania wanaoishi nje ya nchi, lakini kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mzanzibari Mkazi, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva na shughuli za kiuchumi," anasema Dk. Chuwa.

Anataja maswali mengine kuwa yatahusu umiliki wa ardhi na taarifa za Teknolojia TEHAMA, taarifa za uzazi na vifo vilivyotokea ndani ya kaya, vya uzazi, hali ya nyumba za kuishi na umiliki wa rasilimali mbalimbali, maswali kuhusu kilimo na mifugo na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Kwa maelezo hayo ya mtakwimu, ni wazi kwamba hakuna swali linalohusiana na dini, ambalo baadhi ya watu wamekuwa wakieneza kwa umma na kutaka wasijitokeze kuhesabiwa. Anasema, tofauti na sensa zilizopita, ya mwaka huu inatarajiwa kuwa bora zaidi, kwa kuwa itakuwa na vitu vipya ikiwamo kutengwa kwa maeneo ya kijiografia ya kuhesabia watu katika ngazi za kitongoji/mtaa.

"Lakini kutakuwa na upatikanaji wa taarifa za kitakwimu katika ngazi za kitongoji, mtaa pamoja na kuwa na mipaka ya kudumu katika ngazi hizo kirahisi kwa kutumia vishikwambi (tablets) kwenye hatua zote za utekelezaji wa sensa kwa lengo la kupunguza gharama," anasema.

Dk. Chuwa anafafanua kuwa kutakuwa na nyongeza ya maswali yatakayowezesha upatikanaji wa taarifa zaidi za kitakwimu ikilinganishwa na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

"Taarifa za kidemografia (umri wakati wa ndoa ya kwanza), maswali yanayohusu ulemavu (kichwa kikubwa na mgongo wazi, kifafa, mbalanga (storiasis) na usonji (autism) yataulizwa," anasema.

## Serikali, EU sasa kuwaonyesha Watanzania ulipo mlo wenye lishe

INATOKA UK.11

Anaeleza kuwa kulingana na takwimu za 2015-16 za Tanzania Demographic Health Survey (TDHS-MIS), asilimia 34 ya watoto chini ya miaka mitano wamedumaa, hali inayoashiria uwepo wa utapiamlo nchini. Asilimia tano ya watoto chini ya miaka mitano wana unyamavu hali inayoonyesha uwepo wa utapiamlo mkali.

Anawashauri wazazi kuwanyonyesha watoto wao kwa muda wa miezi sita bila kuwapa chochote kama inavyoshauriwa na wataalam ili kuwapa kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Mradi wa AGRI-CoNNECT unaonyesha juhudi mbalimbali za serikali kwa kushirikiana na wadau wa EU na FAO wanaopambana kupunguza tatizo hili na kuweka mikakati na mipango mbalimbali ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata mlo wenye lishe bora.

Tanzania ni moja ya nchi zilizo na ardhi yenye rutuba, mabonde na mito tena taifa linalima vyakula na matunda ya kila aina katika maeneo mbalimbali na hivyo kujitosheleza kwa chakula cha mwaka mzima.

Pamoja na kujitosheleza kwa chakula uzingatiaji wa lishe bora imekuwa tatizo kubwa. Mfano Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Iringa, Njombe, Mbeya, Rukwa na Katavi pamoja na kwamba ndiyo inayoongoza kwa kuwa na chakula kingi lakini inayoongoza kwa matatizo ya ukosefu wa lishe bora. Udumavu wa watoto chini ya miaka mitano kwa sababu ya kula aina moja ya mlo ni mtindo uliyozoeleka kwa kaya nyingi kwenye mikoa hiyo.

Ukitembelea miji mbalimbali mikubwa na midogo kuna ongezeko kubwa la watu wenye unene na uzito uliopitiliza na udumavu miongoni mwa watoto chini ya miaka mitano, yote yakiashiria ulaji duni.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ndivyo miji inavyotisha kiudhalilishaji kinamama

RIPOTI ya ukuaji miji inayotolewa na Benki ya Dunia inatoa angalizo kuwa miaka 25 ijayo, idadi ya watu wanaoishi mijini na majiji barani Afrika itaongezeka maradufu. Ni kutokana na watu wengi kukimbia kuishi vijijini.

Aidha, kufikia mwaka 2040, Tanzania kama yalivyo mataifa mengi ya Afrika raia wake wengi watakuwa wanaishi mijini na majijini na sababu mbalimbali kuelezea hali hiyo zinatolewa mfano, mabadiliko ya tabianchi, ukame, vimbunga yote yakizorotesha kilimo. Pia, mijini kuna matumaini ya kupata kazi, elimu na maisha bora na kwa nchi nyingine migogoro ya vurugu za kisiasa zinahusishwa.

Changamoto kubwa inayoikabili Afrika ni kukua kwa miji kunakoambatana na idadi kubwa ya watu, yote hayo wanawaumiza zaidi wanawake na watoto kwa kuwa masuala ya usawa wa kijinsia na maendeleo ya miji kwenye kutoa huduma za kijamii hayajawajali wanawake na watoto.



Vurugu za usafiri mijini zinawaathiri zaidi wanawake ambao wakati mwingine wanalazimika kupitia madirishani. **PICHA: SABATO KASIKA**

### MIJI ISIYOWAJALI

Wakati wengi wanahamia mijini na majijini maisha salama na bora kwa wanawake na watoto kwenye maeneo hayo ni kitendawili kigumu.

Licha ya kuujua ukweli kuwa upangaji na utoaji wa huduma za kijamii mijini na vijijini hauna mrengo wa kijinsia kwa miongo kadhaa, mambo yamekwenda tofauti na uwekezaji wa kuboresha huduma unabakia kuwa usio wa haki kwa wanawake na watoto ambao mara nyingi wameendelea kuumizwa.

### UNYANYASAJI KIUSAFIRI

Mathalani Dar es Salaam, kubanana kwenye usafiri wa umma daladala na mabasi yaendayo haraka ni jambo linaloweza kusemwa halina tiba.

Kujazana na kubanana kupindukia kunasababisha kudhalilisha wanawake na wasichana kunakofanywa na abiria wanaume.

"Kwenye mwendokasi watu wanabanana kupindukia, kadhalika ndani ya daladala hasa wakati wa matatizo ya usafiri. Tunajiuliza kwanini sheria hazifuatwi? Anasema Grace Mpole, mfanyabiashara wa rasta Kariakoo- Dar es Salaam.

Malalamiko ya abiria na raia ni mengi na ukiyatazama tatizo linaweza kutokana na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kutokusimamia sheria kikamilifu anasema Hassan Mchanjama, Mwenyekiti na mwasisi wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA).

Anatoa maelezo hayo, anapoulizwa na Nipashe kuhusu kuangalia eneo la abiria kubanana na wanawake kudhalilishwa ndani ya vyombo vya usafirishaji wa umma ambalo miji inaelekea kushindwa kulitatua.

"Kwa sheria za usafirishaji mhusika anapokwenda LATRA, anaulizwa kuhusu ruti anayosajili kama ni mijini au mkoa upi kwa mabasi ya masafa. Kadhalika idadi ya abiria ni swali analoulizwa anataja ana apewa leseni za usafirishaji akielezwa kuhusu ruti na nauli halali lakini kwenye kuangalia na kusimamia idadi ya abiria LATRA hawaonekani kufuatilia, hata polisi nao hawalitazami hilo," anasema Mchanjama.

Anawataka LATRA kufuatilia kama wanavyofanya Mamlaka ya Usimamizi wa Maji na Nishati (EWURA) kusimamia gharama za mafuta, bei halali vituoni, kupambana na uchakachaji, vivyo hivyo LATRA nao wawajibike kulinda masuala kama idadi ya abiria, ruti na nauli halali, wasidhani pengine ni jukumu la polisi.

"Tunapata malalamiko ya unyanyasaji na udhalilishaji wa abiria kwenye mabasi ya mwendo kasi kila siku. Tunadhani ni wakati wa kuangalia na kusimamia sheria na kupunguza malalamiko ya abiria na kudhibiti unyanyasaji," anashuri Mchanjama.

### UDHALILISHAJI KILA KONA

Mchanjamana anataja kuwapo malalamiko ya kubanana na kudhalilisha wanawake kwenye meli, vivuko, treni mathalani ya Dar es Salaam hadi Mpanda.

Mwenyekiti wa CHAKUA, anasema malalamiko mengine ni wanawake kuibiwa, kukaa muda mrefu vituoni wakati wanaume wanapandia madirishani na kujaza nafasi wakiwaacha wanawake, watoto na wanafunzi kukesha muda mrefu vituoni.

### 'KULIPISHWA CHOO'

Ukosefu wa usawa wa kijinsia ambalo ni tatizo la kihistoria lipo kwenye vyoo, ambayo ni huduma muhimu lakini haitoshi wala haijasambaa kufikia watu wengi na choo kinatumiwa kwa kununua huduma hiyo. Katika dunia yenye usawa huduma ya choo inatakuwa kupatikana bure.

> "Tunapata malalamiko ya unyanyasaji na udhalilishaji wa abiria kwenye mabasi ya mwendo kasi kila siku.

Wanawake wanaweza kuwa wahitaji wakubwa wa huduma hiyo kutokana na maumbile, lakini miji mingi haijalitambua hilo.

Wakati kinababa wanaweza kumaliza haja zao kwenye ukuta wa uzio, chini ya mti, ndani ya mitaro ya barabara au kwenye nguzo za TANESCO wanawake hawana pakukimbilia.

Ni ukweli kuwa kukosekana vyoo vya kutosha mijini na vinavyotoa huduma bure ni changamoto kubwa zaidi kwa kinamama na wasichana.

Wanawake wanaotembea na watoto wagonjwa wanaohitaji kujisaidia, inapotokea yuko Mbezi stendi ya daladala ni wazi wengi hataweza kumpeleka mtoto anayesumbuliwa na tumbo chooni kutokana na gharama kubwa za Shilingi 500 ili kuingia.

Ili kuondoa tatizo hilo Halmashauri za Miji zijenge vyoo vya watoto wakiwamo wanafunzi wanaokuwa vituoni ambao wazazi wao wanawapa Shilingi 1,000 pengine kwa Dar es Salaam ili kulipa nauli ya 250 kwenda na kurudi na 500 kununua chochote cha kula.

"Haiwezekani kuingia chooni hata kama unabanwa na haja ukiwa kwenye kituo cha mabasi hatuna Shilingi 300 au 500 za kulipa huduma ya choo " anasema Jessey Tesha mwanafunzi wa Sekondari ya Kibweheri anayeishi Mbezi Lousi.

Wanafunzi wanataka huduma bure za choo kwa sababu dharura za kutumia choo zinaweza kutokea wakati wote hata kama mtumiaji hana hela, akibanwa na tumbo, kwa mabinti wakipata changamoto za hedhi yote hayo yanahitaji suala hilo kuangaliwa upya.

Upangaji wa miji na utoaji wa huduma zikiwamo za usafiri ulikosa usawa wa kijinsia kihistoria tangu wakati wa ukoloni na sasa umekuwa ukichangiwa na sera za uliberali hasa mijini ambako kila kitu kinategemea nguvu ya soko na huduma karibu zote zinauzwa.

Mfano huduma zilizoanzishwa kikoloni ni za treni ya abiria ikiwa na mabehewa ya wasafiri wenye fedha nyingi wa daraja la kwanza, la pili na la tatu hubeba mafukara wanaobanana muda wote.

Hata leo miaka 62 ya Uhuru hakujawa na mabadiliko ya huduma ya mabehewa mfumo ni ule ule hivyo ni wakati kufikiria kuwa na mabehewa ya wanawake na watoto kwenye treni hizo.

Bidhaa (huduma) za umma ni adimu katika miji na majiji ni duni mifano wanawake wengi wanaishi katika makazi yasiyo rasmi, wanafanya kazi maeneo hatarishi, hasa katika sekta isiyo rasmi lakini wanaporwa, kujeruhiwa kila siku kutokana na kukosekana ulinzi na usalama wa kijamii kwenye mitaa mingi mijini.

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Wajasiriamali wawa mashujaa, kugeuza matatizo kuwa fursa

WAJASIRIAMALI 178 kutoka Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, wako mbioni kuanzisha vitega uchumi mbalimbali kuanzia uzalishaji wa bidhaa zinazotumia teknolojia rahisi hadi kutengeneza bidhaa za viwandani kama jiki, baada ya kuhitimu mafunzo ya ubunifu ya kugeuza changamoto kuwa fursa.

Ni wa kutoka kata zote 36 za Ilala ambao wanajivunia utaalamu walioupata hivi karibuni kuwa utawawezesha kuwa wabunifu wa kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kuongeza tija kwao na taifa.

Ni hivi karibuni, wajasiriamali hao ambao ni wanachama wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM wamejengewa uwezo na wataalamu kutoka Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam wakipigwa msasa wa jinsi ya kutoboa na kufanikiwa kiuchumi.



Wajasiriamali wakifurahia mafunzo kwa vitendo. **PICHA: SABATO KASIKA**

Mafunzo hayo yametolewa kutokana na kile kinachoelezwa kuwa ukosefu wa ubunifu na elimu ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha harakati za baadhi ya watu ya wanaotamani kupiga hatua katika shughuli mbalimbali.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, anaitaja mafunzo yaliyotolewa na wataalamu wake kuwa jinsi ya kutengeneza bidhaa mbalimbali, lakini kugeuza changamoto kuwa fursa za kuwawezesha kupiga hatua kimaendeleo.

"Tumewafundisha jinsi ya kutengeneza keki na kuipamba, kuzalisha mkaa unaotokana na takataka mbalimbali, sabuni za kufulia, jiki, sabuni za kusugulia masinki, kuoka mikate bila mafuta," anasema Bishagazi.

Anaongeza kuwa wamefunzwa kutengeneza urembo wa aina mbalimbali kwa kutumia shanga na pia wametoa mafunzo ya kufuga kuku, mbinu za kufanya biashara za kuwasaidia watu kuendesha maisha yao kwa ufanisi.

**MSUKUMO WA MAFUNZO**

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Ilala, Mohamed Msofe, anasema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kutaka wanachama hao kupata ujuzi na kuupeleka katika vikundi vyao ili vipige hatua kwenda mbele.

"Kumekuwapo na baadhi ya wanawake wanaochukua mikopo inayotolewa na manispaa bila kujipanga na kujikuta wanaitumia kwa mambo mengine, ndiyo maana tukaamua kuandaa mafunzo haya," anasema Msofe.

Anafafanua kuwa jumuiya hiyo imeandaa baadhi ya wanachama wake na kuwapeleka katika mafunzo ili wapate ujuzi utakaowasaidia katika biashara zao, lakini wakausambaze kwenye vikundi vingine.

"Ninaamini kuwa mafunzo ambayo wanachama wetu wamepata kutoka kituo hiki, watayatumia kikamilifu kuanzia katika biashara ili fedha za mikopo watakazopata zisipelekwe kwenye mambo mengine," anasema.

## WANENAVYO MALENGA

### TUTAKULA NA KULIPA

Twabanana hapahapa, tutakula na kulipa,
Hata kama ni makopa, tutatafuna mfupa,
Wengine hapa wakwepa, kwa wengine panalipa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Kijini wanakwepa, kulima wanaogopa,
Mimi niko hapa hapa, kilimo kwangu chalipa,
Watu wa ugani hapa, miongozo wananipa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Eti mjini kwalipa, jinsi wanachapa lapa,
Huo naona mfupa, mgumu fisi asepa,
Hasa bila kazi hapa, shibe inakuwa kapa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Ni kawaida nakopa, na muda wake nalipa,
Siyo wewe unakopa, na kulipa unakwepa,
Unakaa kuongopa, kwamba kesho utalipa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Maisha yetu ni hapa, uking'ang'ana yalipa,
Na umeme upo hapa, habari michezo supa,
Maji yasogea hapa, hata sipitali hapa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Serikali inalipa, inakopa na kulipa,
Huduma zile yatupa, nchi inakuwa supa,
Elimu ya kwetu hapa, inazidisha kulipa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Lakini kweli yalipa, imetufikisha hapa,
Na walimu wetu supa, hata kama wanachapa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Sikai nikaongopa, na maisha kuogopa,
Yafanywayo yanalipa, amua wewe kusepa,
Na walimu wawa supa, hata kama wanachapa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Maisha ni hapa hapa, wala siyo ya kukopa,
Ya kwao kama yalipa, waliikaza mishipa,
Wala hawakuogopa, nawe acha kuogopa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

Changamoto yetu hapa, yatoka kwao si hapa,
Bei za mafuta hapa, kwetu mgumu mfupa,
Zaleta ugumu hapa, tusipae kama chopa,
Mambo ya kutapatapa, yamefika mwisho hapa.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### KUNA MBWEHA WASUBIRI

Tufurahie maisha, kama tunayo maisha,
Tusiishi kujichosha, na kujidharaulisha,
Jasho letu latutosha, familia kuwezesha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Wewe ndiwe wazalisha, juhudi zako zatosha,
Mkeo hujamwonyesha, njia unaifupisha,
Hao wawaaminisha, wadhani watakutosha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Malaika wakukosha, mali zenu mwazungusha,
Unavyojifikirisha, wanavyofaa watosha,
Kumbe wajifikirisha, jinsi watavyokuosha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Sifanyi kukufundisha, jinsi kuishi maisha,
Lakini nakukumbusha, unajisahaulisha,
Wakukufaa maisha, familia wanatosha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Hata dini zafundisha, wafaao kimaisha,
Hao wa kuwarithisha, mali ulizozalisha,
Hayo hasa ni maisha, si wengine kuwalisha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Lini watalianzisha, yakikatika maisha,
Jeneza watalifikisha, kaburini kudondosha?
Au mada taanzisha, kaburi hawajachimbisha?
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Hivyo ulivyozalisha, katika yako maisha,
Mgongo ulipindisha, kijasho ukadondosha,
Misuli ulitunisha, malengo ukafikisha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Mwenzi wako hakikisha, akujua kimaisha,
Vyote ulivyozalisha, kuwekeza wahusisha,
Mungu akikutowesha, watoto atawalisha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Wosia kutayarisha, jambo la kufurahisha,
Ukimaliza maisha, ujumbe watafikisha,
Hakuna kuhangaisha, na ngumi kuvurumisha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

Tufurahie maisha, Mungu akitudumisha,
Wategemezi husisha, uweze kuwawandisha,
Mungu akikutowesha, waendeleze maisha,
Kuna mbweha wasubiri, ufe wagawane mali.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



# Zimamoto yataka taarifa za moto zitoke mapema

Na Renatha Msungu, DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Dodoma, limewataka wananchi kutoa taarifa mapema ya matukio ya moto yanapotokea katika maeneo mbalimbali ili kuepuka kutokea madhara makubwa.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambaye pia ni Kamanda wa Zimamoto Mkoa wa Dodoma, Julishaeli Mfinanga, alisema hayo wakati wa kilele cha Wiki ya Zimamoto inayoazimishwa Mei kila mwaka duniani.

Kamanda Mfinanga alisema kufanyika kwa maadhimisho ya Wiki ya Zimamoto ulimwenguni kote kila mwaka kumekuja baada ya nchi ya Australia kupoteza askari wake wanne mwaka 1999 kutokana na janga la moto wakati wanapambana na tukio la moto.

Alisema kutokana na utafiti waliozifanya za matukio ya moto zimeonyesha aliyeunguliwa siye anayepiga simu bali wanaotoa taarifa za kutaka msaada wa kusaidiwa kuokolewa ni wapita njia wakiwamo majirani.

Aliwataka wananchi kuwa na namba za dharura ili iwe rahisi kwao kupiga pale wanapopatwa na majanga ya moto au matukio mengine.

Alisema kuwa jeshi hilo halijawahi kuchelewa katika eneo la tukio la uokoaji na kwamba wakipata taarifa kwa wakati inawasaidia kufika haraka kwenye eneo la tukio.

Aidha, kamishna huyo alifafanua kuwa magari ya zimamoto yanauwezo mdogo wa kubeba maji na sio Tanzania tu bali hata nchi za nje.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kutambua kuwa jeshi hilo linafika kwa wakati huku wakiwa na maji tatizo lililopo ni magari yana uwezo mdogo wa kubeba maji ambapo hubeba lita 6,000 hadi 7,000 ambazo huisha kwa haraka.

"Kumekuwa na malalamiko ya kutofika kwa wakati katika matukio, si kweli tunafika kwa wakati isipokuwa changamoto ni magari hubeba maji madogo," alisema Kamanda Julishaeli.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mnadani, Joyce Kaishozi, alisema elimu ya zimamoto wanayoitoa shuleni hapo na kitabu cha uraia na maadili cha darasa la saba kina mada ambayo ni elimu ya zima moto na uokoaji katika jamii.

Kashozi alisema kitabu hicho kinaeleza hatua za uzimaji moto na uokoaji na jeshi hilo limeenda sehemu sahihi ya kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Akitoa elimu ya uokoaji Ofisa Habari Uhusiano na Elimu kwa Umma, Sajenti Joyce Kapinga, alisema wanamajukumu mbalimbali katika jamii ya uokoaji kama vile majanga ya moto, majini ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya afya kwa jamii hiyo.



Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Tanzania PlC, Linda Riwa (katikati), akiulizia maendeleo ya Shule ya Msingi Mango iliyoko wilayani Kibosho, mkoani Kilimanjaro wakati timu ya watendaji waandamizi walipotembelea miradi kwenye shule hiyo, watatu kushoto ni Mkurugenzi wa Vodacom, Rosalynn Mworia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za dini, wadau waombwa kuziwezesha jamii zisizojiweza

Na Peter Mkwavila, DODOMA

TAASISI za kidini na wadau wa maendeleo wametakiwa kuzisaidia jamii zisizojiweza katika nyanja mbalimbali kama vile ya afya, elimu, chakula, mavazi na uchumi ili kuziwezesha kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Rai hiyo ilitolewa juzi na mwangalizi wa kanisa la Talitha Cumi Daniel Kitua, wakati alipokuwa akikabidhi kadi za bima za afya kwa watu wasiojiweza zaidi ya 75 wakiwamo wazee wasiojiweza na wenye ulemavu kutoka kata ya Tambukareli jijini Dodoma.

Kitua, alisema taasisi za kidini na wadau wa maendeleo wanawajibu wa kusaidia jamii isiyojiweza badala ya kuona suala hilo ni la serikali peke yake na wafadhili kutoka nje ya nchi.

Alisema kadi hizo la bima ya afya zilizotolewa na kanisa hilo zimelenga kuwasaidia katika kupunguza gharama za kupata matibabu kwenye vituo vya afya vinavyotoa huduma za kiafya.

"Kanisa la Talitha Cumi, limeona liwasaidia wazee hao na watu wanaoishi katika mazingira magumu kadi za bima ya afya, ili kuwapunguzia gharama kubwa ya matibabu pale wanapokwenda kupata matibabu kwenye vituo vya afya," alisema.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Tambukareli Jiji la Dodoma, Juma Mazengo, alisema serikali bado inathamini na kutambua mchango mkubwa unaofanywa na taasisi za kidini na wadau wa maendeleo kwa kuhakikisha wanaisaidia katika kutoa misaada yake kwa jamii isiyojiweza.

Mazengo, alisema kuwa kitendo kilichofanywa na kanisa la Talitha Cumi kinatakiwa kuigwa na taasisi zingine za kidini ili ziweze kuwafikia walengwa walio wengi ambao wanakabiliana na maisha magumu kila siku.

Mdau wa maendeleo, Elice Yohana, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kuwa msaada huo utawasaidia wasiojiweza kuokoa afya na maisha yao.

Alisema bado kuna ulazima wa kuiangalia jamii hiyo yenye uhitaji, ili wafikiwe na waweze kuondokana na kero wanazozipata katika afya, elimu, chakula na mavazi. Awali akizungumza kwenye ibada ya kukabidhi kadi za bima ya afya Askofu Mkuu wa huduma ya The Word of Prophec Ministry Tanzania, John Mwakilemi, aliwakumbusha Watanzania kuwa na umoja na upendo.

Alisema kuwa Watanzania wakiwa na upendo na umoja wataweza kuikumbuka jamii hiyo ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi.

## Prof: Mkenda: Taifa linahitaji elimu bora

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema taifa linahitaji elimu bora na si bora elimu kwa kuongeza ubunifu katika maeneo ya kujifunzia ikiwamo kutoa hamasa kwa walimu ili kuwaongezea morali.

Prof. Mkenda alisema hayo wakati akifungua hafla fupi ya kuwatunuku walimu mahiri bakishishi ya kushiriki mradi wa Kiufunza mpango wa tatu (2019-2021) iliyoandaliwa na TWAWEZA kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na TAMISEMI.

Prof. Mkenda alisema kukiwa na walimu wenye ubora ni lazima elimu itakuwa bora, hivyo ameipongeza TWAWEZA kwa kuja na mradi wa Kiufunza ambapo itachochea kila mwalimu kuongeza ubunifu katika kazi yake awapo darasani.

"Nawapongeze sana TWAWEZA chini ya Mkurugenzi, Aidan Eyakuza kwa ubunifu huu kwa sababu matarajio yetu kama wizara ni kuiweka elimu juu, hivyo TWAWEZA mmesaidia kuonyesha njia kwa vitendo," alisema Prof. Mkenda.

Hata hivyo alisema katika kuhakikisha maboresho ya elimu yanafanyika hivi sasa ambapo wizara inaendelea kupitia baadhi ya sera, sheria na mitaala iliyopo ikiwezekana kupunguza au kuongeza mambo muhimu ili kufanya elimu iendelee kuwa bora.

Alibainisha kuwa ili kuhakikisha kuna kuwepo na mazingira salama ya kujifunzia na kufundishia (miundombinu na vitendea kazi) katika hili serikali imeshapiga hatua kubwa sana na kuongeza agenda ya sasa ni kuhakikisha sera, sheria, mitaala, miundombinu pamoja na vitendeakazi vinaboreshwa.

Katika hatua nyingine, alisema katika kuhakikisha kuwa ubora wa elimu unakuwepo nchini wameandaa mkutano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwezi ujao, ambapo mawaziri wa elimu na wataalamu wa sekta ya elimu kutoka mataifa mbalimbali duniani ikiwamo Ureno, Pakistan, Afrika Kusini, Kenya, Sierra Leone wanatarajia kushiriki.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuzungumzia ubora wa elimu ikiwamo kupata uzoefu wa mataifa mengine katika sekta ya elimu.

**"Nawapongeze sana TWAWEZA chini ya Mkurugenzi, Aidan Eyakuza kwa ubunifu huu kwa sababu matarajio yetu kama wizara ni kuiweka elimu juu, hivyo TWAWEZA mmesaidia kuonyesha njia kwa vitendo," alisema Prof. Mkenda.**





# Wazazi wanaowanywesha watoto pombe kukiona

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

MKUU wa Wilaya Ileje, mkoani Songwe, Anna Gidarya, amepiga marufuku wazazi na walezi wanaowanywesha pombe za kienyeji watoto wadogo na kushinda nao vilabuni na kwamba yeyote atakabainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Gidarya alitoa marufuku hiyo mwishoni mwa wiki, alipozungumza na wakazi wa wilaya hiyo kwa lengo la kusikiliza na kutatua vikwazo vinavyowakabili.

Alisema kumekuwa na wimbi kubwa la wazazi kwenda na watoto wao wadogo vilabuni kunywa pombe na wakati mwingine huwanywesha ili wasisumbue wakati wakiendelea kunywa.

Alisema tabia hiyo inafanywa zaidi na wanawake na kwamba madhara ya vitendo hivyo ni kusababisha udumavu kwa watoto na baadae kuzalisha kizazi chenye uelewa mdogo wa mambo.

Kutokana na hali hilo Gidarya aliagiza watendaji wote wa Kata 18 za Wialaya hiyo, kufanya misako kwenye vilabu vyote vya pombe za kienyeji ili kuwakamata wanawake wote wanaofanya vitendo hivyo.

"Msako wa kuwakamata wanawake wote wanaokwenda na watoto vilabu vya pombe uanze mara moja haiwezekani tuone watoto wetu wasio na hatia wanapata madhara ya kiafya kwa sababu ya ujinga wa wazazi wao, mnapenda kuona afya za watoto zinadhoofu na kupata udumavu sio," alisema Gidarya.

Aidha, aliwasisitiza watendaji wa kata kufanya vikao vya mara kwa mara kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhusu athari za matumizi ya pombe kwa watoto wadogo na kuwasababishia udumavu na kwamba elimu hiyo iwe endelevu.

Aliongeza kuwa kuanzia mwezi Julai mwaka huu, shule zote za msingi na sekondari, viongozi wa vijiji kwa kushirikiana na kamati za shule kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula cha mchana shuleni ili kusaidia kuongeza kiwango cha ufaulu pamoja na kuondoa udumavu.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ileje, Pastori Mashiku, alisema kila mtendaji wa kijiji na kata kwa kushirikiana na kamati za afya kuendelee kutoa elimu ya lishe kupitia mikutano ya hadhara ili kila mwananchi achukulie uzito lengo likiwa ni kutokomeza tatizo la udumavu wilayani humo.

Miongoni mwa wakazi walioshiriki mkutano huo akiwamo, Esther Kamendu ambaye ni mkazi wa kijiji cha Mbebe alisema kinamama wameona ni kawaida kwenda vilabuni na watoto wadogo, hivyo agizo la kuwakamata litakuwa limenusuru afya za watoto kwani hunyweshwa pombe wakiwa na umri mdogo.

Marko Mbwagha alisema wazazi wengi hawazingatii elimu ya lishe wanayopewa kuanzia kipindi cha ujauzito hadi kujifungua na badala yake kuamua kuwanywesha pombe watoto wao hivyo watakaokamatwa watakuwa mfano kwa wengine.

Imeelezwa kuwa Mkoa wa Songwe unashika nafasi ya tatu kutokana na tatizo la udumavu kwa asimilia 43.3 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano licha ya kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa chakula nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, akishiriki zoezi la upandaji miti katika Zahanati ya Igawa juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Waziri awaahidi tuzo walimu watakaofaulisha kiwango cha alama A

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Tunduma mkoani Songwe, David Silinde, amewahidi walimu wote wa shule za msingi na sekondari watakaofaulisha wanafunzi kwa alama A kupewa tuzo.

Silinde alitoa ahadi hiyo juzi, wakati wa hafla ya kuwapongeza walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani yao ya kidato cha nne, pili, darasa la nne, shule bora na walimu bora, ambazo ziliandaliwa na Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa jambo hilo katika kuongeza motisha ya kufundisha na kuongeza ufaulu kwa watoto, Silinde aliwaahidi kuboresha tuzo hizo ili mwakani ziwe bora walimu, shule na wanafunzi wafurahie.

"Nawapongeza wadau wa elimu wakiwamo madiwani wa Mji wa Tunduma kuridhia kuanzishwa kwa tuzo za elimu ambazo naaimani zitapaisha jimbo letu kupata matokeo mazuri ya mitihani ukilinganisha na ilivyokuwa awali," alisema Silinde.

Aidha, alisema katika kufanikisha utoaji wa tuzo msimu ujaoa wataongeza wigo wa kushirikisha wadau ili zawadi zitakazotolewa ziongeze chachu ya ufaulu wa mitihani kwenye jimbo hilo.

Aliwasisitiza walimu wote katika mji huo kuongeza kasi ya kufundisha wanafunzi kwa kuhakikisha wanamaliza mitaala yote kwa wakati ili muda unaobaikia hususani kwa madarasa ya mitihani wapatiwe mazoezi ya kutosha ili kujipima na kujua mambo ya kuyashughulikia kabla ya kuanza mitihani ya kitaifa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Magesa Philemon, alisema wataalamu na madiwani wa mji huo wamejipanga kuhakikisha matokeo ya mitihani ya kitaifa yatakuwa mazuri ukilinganisha na ilivyokuwa awali.

Alisema waliamua kuanzisha tuzo hilo kwa lengo la kuongeza ufaulu na kwamba motisha inaweza kuchochea walimu na wanafunzi kufanya vizuri na kuupaisha mji wa Tunduma kielimu.

# Sekta ya ujenzi eneo hatarishi kazini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UTAFITI ambao umefanywa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), unaonyesha kuwa sekta ya ujenzi ndiyo inayoongoza kwa kuwa eneo hatarishi zaidi mahali pa kazi.

Kutokana na hatari hiyo, makandarasi wanaotekeleza miradi ya ujenzi wamekumbushwa kuongeza umakini na kuchukua tahadhari ya kulinda usalama wa wafanyakazi wao.

Matokeo ya utafiti huo yalitolewa juzi na Meneja wa Mafunzo wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi, Mhandisi Shaban Mbaga, wakati akitoa mafunzo ya usalama mahali pa kazi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), wanaosomea uhandisi wa ujenzi, barabara na migodi.

"Kwa kutambua athari wanazoweza kupata makandarasi hao, wameanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi wanaosomea masomo ya uhandishi ili kuwafundisha namna bora ya kujiepusha na madhara pindi wanapotimiza majukumu yao kuanzia kwenye mafunzo ya vitendo hadi watakapohitimu na kupata ajira," alisema Mbaga.

Alisema baada ya kubaini tatizo ya ukosefu wa ujuzi katika kukabiliana na majanga wawapo kazini, OSHA inaendesha mafunzo kwa wanafunzi wahandisi ili kutimiza majukumu yao kwa tahadhari.

Kutokana na matokeo hayo ya utafiti, baadhi ya wadau akiwamo Idris Kassim, waliiomba serikali kuanzisha pragramu maalum ambayo itawajengea uwezo wanafunzi kujua namna bora ya kujiepusha na madhara wanapotimiza majukumu yao.

Wanafunzi wa Must, waliitaka serikali kuongeza msisitizo na kutoa kipaumbele cha usalama kuanzia mahali pa kuishi wananchi mpaka maeneo yao ya kazi.

Aman Massawe alisema mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka ambapo wanafunzi hao wanakaribia kwenda kwenye mafunzo ya vitendo na kwamba watayatumia vyema kwa usalama wa maisha yao.





## 'Mwamko wa wanaume kuongozana na wenza wao kliniki bado mdogo'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, amesema kuwa bado mwamko ni mdogo wa wanaume kuongozana na wenza wao kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito.

Mazrui alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi Zawadi Amour Nassoro wa Jimbo la Konde Pemba aliyetaka kujua kwa nini wanaume wengi hawapo tayari kufuatana na wake zao wakiwa wajawazito kwenda kliniki kuchunguza afya zao.

Alisema licha ya wataalamu wa afya kuhimiza wanaume kuongozana na weza wao kufika kliniki kuchunguza afya zao lakini bado wengi wao hawapo tayari hasa wake zao wanapokuwa wajawazito.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Afya ni kuwahamasisha wanaume kuwa tayari kuwaunga mkono wanawake katika kufika hospitali na kuchunguza afya zao kabla ya kujifunguwa ili kuwa salama zaidi.

"Mheshimiwa nawaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waonyeshe mfano wa kuigwa kuwasindikiza wake zao kwenda kliniki kuchunguza afya ili waweze kujijuwa afya zao mapema," alisema.

Alieleza mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuimarisha afya za wajawazito ili kujifungua salama na kupunguza vifo vinavyotokana na watoto.

Alieleza kuwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja imetoa ruhusa ya kinababa kushuhudia wake zao wanapojifungua wakiwa katika wodi maalum lakini ni wachache wanaofanya hivyo.

"Tumeweka wodi maalum ya kinamama wanaojifungua kama kuna baba anataka kushuhudia kitendo cha mke wake kujifungua ili kuona machungu anayopitia, lakini wanaume hawaendi huwaacha wanawake pekee kupitia machungu ya kujifungua," alisema Mazrui.

# SMZ yaanza kuchukua hatua kuokoa kisiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema kuwa Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na mwekezaji kutoka Afrika ya Kusini wameanza kuchukua hatua za kukiokoa kisiwa cha Mnemba kiliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ambacho kipo katika tishio la kutoweka kutokana na kasi ya mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizowasilishwa na wajumbe wa baraza hilo waliochangia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake katika uwekezaji.

Soraga alisema kisiwa cha Mnemba kimekodishwa kwa wawekezaji kutoka Afrika Kusini ambacho ni maarufu kwa kutembelewa na watalii mbalimbali maarufu duniani.

Alisema juhudi mbalimbali zimeanza kuchukuliwa katika kukabiliana na tishio la kisiwa hicho kupotea katika ramani ya visiwa vilioko Zanzibar ikiwamo kulinda maeneo ya pembezoni mwa fukwe.

Aidha, alizitaja baadhi ya sababu ambazo zimechangia kuwapo kwa athari za mazingira katika kisiwa hicho ikiwamo shughuli za uvuvi wa kuzamia baharini unaofanywa na wananchi wanaoishi katika maeneo jirani ya kisiwa hicho.

Aidha, alisema kisiwa hicho kipo katika eneo la bahari karibu na mwamba kwa hivyo kimekuwa kikishambuliwa na kasi ya mawimbi ya baharini na hivyo kusababisha mmong'onyoko pembezoni mwa fukwe na kuzowa mchanga.

"Kisiwa cha Mnemba muundo wake ni kama fungu kikiwa kimezungukwa na mchanga ambapo mawimbi makali ya baharini huchukuwa mchanga na kusababisha tishio," alisema.

Waziri huyo alisema serikali pia itaendelea kuhamasisha wawekezaji wazalendo kuwekeza ambao wamepewa kipaumbele cha kwanza kuona wanaitumia fursa hiyo muhimu kukuza uchumi na pato la taifa.

Alisema mwenyeji anayetaka kuwekeza katika sekta ya utalii anapaswa kuwa na kima cha mtaji usiopungua dola za kimarekami 300,000 wakati mgeni atalazimika kisheria awe na mtaji usiopunguwa dola za kimarekani 2,500,000.

Aidha, alizitaja fursa nyingine zimetajwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA) ambazo zinapatikana kwa wenyeji pekee ikiwamo kuongoza kampuni za kutembeza watalii nchini au kumiliki.

Aliwataka wananchi wazalendo na wafanyabiashara kujitokeza kuchangamkia fursa hizo za uwekezaji ili waweze kuchangia pato la taifa katika sekta hiyo yenye ukuaji mkubwa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi wataka KMKM kuongezewa bajeti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametaka bajeti ya Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) iongezwe kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya baharini pamoja na kuimarisha doria katika ukanda wa pwani ya visiwa vya Zanzibar.

Walibainisha hayo walipokuwa wakichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ kwa mwaka wa fedha 2022-2023, na kueleza kuwa kikosi hicho kinakabiliwa na majukumu makubwa ambayo ni ulinzi wa doria katika maeneo ya bahari mwambao wa visiwa vya Zanzibar katika kukabiliana na uhalifu.

"Hivi sasa Zanzibar imeunda mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya ambayo itakuwa na kazi ya kufanya doria katika maeneo yote ya mwambao wa bahari ya Zanzibar," alisema Mwakilishi wa Tumbatu, Haji Omar Kheir.

Haji alisema ili kufanikisha malengo hayo suala la upatikanaji wa vyombo vya kufanya doria unahitajika ili kuona matukio ya uingizaji wa dawa za kulevya unadhibitiwa kikamilifu.

"Mheshimiwa Spika kikosi cha KMKM ni muhimu ambapo majukumu yake yanahusiana na doria katika mwambao wa visiwa hivi ambapo tunahitaji kuongeza bajeti kwa ajili ya kudhibiti ulinzi," alisema.

Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, alipongeza kikosi hicho ambacho sasa kimeongeza majukumu yake ya kuingia katika uvuvi wa bahari kuu na kuvuna rasilimali za baharini.

Alisema wakati umefika sasa kikosi hicho kuongezewa bajeti yake kwa kukiwezesha kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufanya doria katika maeneo ya mwambao wa pwani pamoja na kupambana na kusaidia kukabiliana na majanga.

Mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf alisema majukumu ya KMKM ni makubwa ambayo ni kulinda amani na usalama wa visiwa vya Zanzibar na matukio ya majanga na uharamia.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022-2023 na kuidhinisha jumla ya Sh. bilioni 205,861,915,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL LONG'IDA SANETI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba. **S0409-0081.**
Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya MORINGE SOKOINE SECONDARY SCHOOL mwaka 2014. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu naye. Polisi taarifa: **ARU/MON/RB/170661/2022.**

---

IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA

CIVIL CASE NO. 26 OF 2021

DAUDI SALAT OGADEN....................PLAINTIFF

VERSUS

JOSEPH NDUGU OCHIENG...........DEFENDANT

ORDER

**BEFORE: B.I. MWAKISU-RM**
Date: 21/04/2022
Coram: B.I. MWAKISU- RM
Plaintiff : present
For the plaintiff: mwale, advocate
Defendant:
For the defendant: Absent
CC:- Fransisca

(Sgd) B.I. Mwakisu- RM

21/04/2022.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GS GROUP LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 812 CYL** yenye chassis namba **LC6PCJK27M0026980.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**SO/RB/1720/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LAMADAI NAMBARI 18/2022**

**MDAI: JAKLINE MATESO**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: WILLIAM AYUBU**
**WA**
**TANZANIA BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 12/05/2022 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.

Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumanne 19 tarehe 04 Mwezi 2022

HAKIMU

PRIMARY COURT MAGISTRATE
GEITA

---

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MAOMBI MADOGO Na.25/2021**
**MDAI: ANASTASIUS MBOGORO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: PHILIPO FELIX**

Kwa mamlaka tuliyopewa na Baraza la Ardhi na Nyumba(W) ya Iringa, tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba ya mdaiwa ya makazi iliyopo Mtwivila "B" katika kiwanja nambari MTW/B/94 na 95 iliyopo katika Manspaa ya Iringa.
Mnada utafanyika tarehe **30/05/2022** siku ya **Jumatatu saa tano kamili(5:000 Asubuhi.**
**MASHARTI:**
Mnunuzi atakayewini atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa na kiasi kilichosalia kilipwe ndani ya siku kumi na nne(14) na akishindwa kulipa nyumba itauzwa tena kwa mnada wa hadhara na malipo ya awali hayatarudishwa.

**MAJEMBE AUCTION MART**
**Kwa mawasiliano piga: 0734 848 485**
**au 0755 976 679 IRINGA.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAMU MPOCHI ALLY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba **S.0528-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SABASABA SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/46475/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOSES MARCO SHEIFUMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Nissan Caravan yenye usajili namba **T 488 DGZ,** CHASSIS NAMBA: **VRMGE24053001,** ENGINE NAMBA: **TD27172509.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/177727/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...TEMEKE**

**Kituo cha..... JUMUISHI.... Mkoa... DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi............784/2022................**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: OMARI SAIDI JUMA NGULUBE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: OMARI SAIDI NGULUBE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 mwezi 05 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 04 mwaka 2022

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Ndugu, AMINA HAMOUD NDEGE**, Anatangaza kupotelewa na Cheti chake cha Kidato cha Sita na Cheti cha Chuo. Kidato cha Sita **Index no S.0306-0503** No ya Cheti **M200778** kilichotolewa na baraza la mitihani katika shule ya Dodoma Sekondary **Mwaka 2015,** Cheti cha chuo cha Tumaini Makumira Mkoa wa Arusha **Mwaka 2018.** Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi DOD/DOD/RB/172656/2022.**

---

*Uza,*
*Chenye Thamani*
*Kubwa Kwa*
*Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie*
*0782253676*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## NMB Teleza Kidijitali yazinduliwa D'Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeanza rasmi kampeni ya kuinadi kampeni ya Teleza Kidijitali iliyozinduliwa Aprili 11 na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jijini Dodoma.

Sasa inapelekwa mtaani, kuwaelimisha wateja na wasiokuwa wateja umuhimu wa huduma zilizo chini ya mwamvuli huo, ambazo ni NMB Pesa Wakala, Lipa Namba na Mshiko Fasta.

Uzinduzi wa kampeni hiyo umefanyika NMB Tawi la Tandika wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, ambako Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, aliambatana na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, kuzindua na kisha kuwatembelea wafanyabiashara madukani ili kuwapa elimu zaidi.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Zaipuna alisema ujio wake yeye na viongozi wengine waandamizi wa NMB Makao Makuu na kuungana na wale wa Tawi la Tandika, umelenga kutoa elimu ya kutosha na kuwaingiza Watanzania wengi zaidi kwenye Sekta Rasmi ya Kifedha ili waweze kunufaika na huduma mbalimbali ambazo wanazitoa.

"Tuko hapa kunadi huduma zote muhimu zilizo kwenye mwamvuli wa Teleza Kidijitali, ambazo ni Mshiko Fasta ambayo ni mikopo nafuu isiyo na dhamana, inayopatikana kwa njia ya simu kwa wateja wenye akaunti, ambako mteja hatahitaji kitambulisho wala dhamana yoyote kuupata.

"Pia tumeutumia uzinduzi wa kampeni hii kwa ujumla kunadi huduma ya Lipa Mkononi, ambayo itamwezesha mfanyabiashara kuitumia kulipwa na wateja wake kwa kutumia namba ya malipo au kuskani QR, huku ikitupa sisi kumbukumbu na historia ya mfanyabiashara ambayo itasaidia hata katika utoaji wa mikopo.

"Pia tumekuja na NMB Pesa Wakala, huduma inayomwezesha mtu yeyote kuwa wakala bila kutumia mashine, ambayo itamwezesha kutoa huduma za kuweka, kutoa ama kutuma pesa kirahisi kwa kutumia hata simu ya kitochi," alisema Zaipuna, ambaye alishiriki kutembelea wafanyabiashara wa eneo la Tandika madukani mwao kutoa elimu na kusikiliza maoni yao.

Zaipuna aliielezea kampeni hiyo kwamba imelenga kuhakikisha wanawapa elimu Watanzania waweze kuwa sehemu ya watumiaji wa huduma za sekta rasmi ya kifedha na kwamba wanaamini NMB Pesa Wakala, Lipa Namba na Mshiko Fasta, vitakuwa chachu ya ukuaji kibiashara na kiuchumi kwa wateja wao kote nchini, ambako wameahidi kuifikisha Teleza Kidijitali.

# Wananchi wapewa ahueni kero ya maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI 4,480 katika kijiji cha Nonwe Kata ya Ubagwe Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wanatarajia kuondokana na tatizo la ukosefu wa majisafi na salama, baada ya wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na serikali kusaini mkataba wa ujenzi wa kisima cha maji chenye thamani ya Sh. milioni 53.

Ujenzi wa kisima hicho umefadhiliwa na kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya JTI na utanufaisha kaya 450 sawa na wakazi 4,480.

Mradi huo unatarajia kukamilika mwezi huu na kuwa suluhisho la tatizo la maji katika kijiji hicho.

Hayo yalibainishwa jana na mwakilishi wa kampuni ya JTI, Joram Charles aliposaini mkataba wa ujenzi wa kisima na usambazaji wa maji katika kijiji cha Nonwe Kata ya Ubagwe kati yake, mkandarasi na serikali.

Alisema ujenzi wa kisima hicho pamoja na usambazaji wa maji utagharimu Sh. milioni 53.

Charles alisema fedha za ujenzi wa kisima hicho zinatokana na faida inayopatikana baada ya kununua na kuuza tumbaku.

Naye Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanule Cherehani, aliwataka wananchi wa Nonwe kuulinda mradi huo wakati serikali ikiendelea na upembuzi yakinifu wa kuleta mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Viktoria ambao utakuwa suluhu ya tatizo ya maji kwa wananchi wa eneo hilo.


Awali akitoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo, diwani wa Kata ya Ubagwe, Robert Mihambo alisema kwa sasa wanatumia maji ya visima na mabwawa ambayo siyo safi na salama kiafya hali ambayo imekuwa ikisababisha kupata magonjwa ya homa za matumbo.

"Tunatumia maji ya mabwawa kwa kuchangia na wanyama aina ya fisi na tembo ambao wanapatikana katika eneo hili, hivyo kupatikana kwa mradi wa maji ya kisima kirefu kutatuondolea adha ya upatikanaji wa maji," alisema Mihambo.

Mkazi mwingine, Ghati Marwa, alisema kuwa wanawake wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 10 kufuata huduma ya maji katika mabwawa yaliyo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Kigosi Moyowosi ambayo siyo safi na salama na wakati mwingine wananusurika kushambuliwa na fisi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Sophia Mjema, aliishukuru kampuni ya JTI kwa kurudisha fadhila kwa wananchi kwa kujenga mradi wa maji na kuzitaka kampuni mengine yanayonunua zao la tumbaku kuiga mfano huo.

Alisema serikali itaendelea kuwaunga mkono katika kazi zao ikiwa ni pamoja na tushirikiana kutatua kero za wananchi hususani za maji.



Mkuu wa Matawi ya Benki ya Exim, Agnes Kaganda (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kuhusu huduma mpya ya bima ya maisha iitwayo 'Pamoja Hadi Mwisho' inayotolewa na benki hiyo kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Alliance Life Assurance mahususi kwa ajili ya vikundi rasmi na visivyo rasmi jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Bima kwa benki za benki hiyo, Melchizedeck Muro (kulia) na Mkuu wa Idara ya Bima kutoka Kampuni ya Bima ya Alliance Life Assurance, Juma Patrice (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Exim yaviwezesha vikundi kwa bima

**Na Mwandishi Wetu**

VIKUNDI rasmi na visivyo rasmi vimepata fursa ya bima ya maisha iliyotolewa na Benki ya Exim Tanzania.

Benki hiyo imezindua huduma mpya ya bima ya maisha iitwayo 'Pamoja Hadi Mwisho' mahususi kwa ajili ya vikundi rasmi na visivyo rasmi, ikilenga kuongeza ushirikishwaji wa jamii zaidi katika kupata huduma hiyo muhimu.

Huduma hiyo inayopewa amana na Kampuni ya Bima ya Alliance Life Assurance inahusisha bima ya maisha kwa vikundi rasmi na visivyo rasmi ikilenga kusaidia vikundi hivyo na wanavikundi dhidi ya majanga yatokanayo na vifo, ulemavu wa kudumu na elimu kwa watoto wanaoachwa pindi mwanachama anapofariki.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Matawi ya Benki ya Exim,. Agnes Kaganda, alisema huduma hiyo inakwenda sambamba na adhma ya serikali katika kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anafikiwa na huduma za bima.

Aidha, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Bima cha Benki ya Exim, Melchizedeck Muro alisema "Mpango huu wa 'Pamoja Hadi Mwisho' umeletwa kwa lengo la kuhakikisha huwaachi nyuma Watanzania linapokuja suala la kujilinda wao, familia zao na wapendwa wao. Ndio maana kupitia mpango huu tumegusa vikundi rasmi na vile visivyo rasmi ikiwamo vikundi vya wafanyakazi, wajasiriamali, vyama vya ushirika, makundi ya mitandao ya kijamii mfano Whatsapp, Facebook, na Telegram na vikundi vingine vya namna hiyo."

Bima ya maisha ya 'Pamoja Hadi Mwisho' Inamlinda mwanachama na familia yake sehemu yoyote na muda wowote walipo ndani ya Tanzania.

Akizungumzia zaidi kuhusu faida za mpango huo, Muro alisema: "Kupitia mpango huu hakuna muda wa kusubiri. Fao litatolewa ndani ya saa 72 baada ya kupokea nyaraka zote za madai. Mwanachama wa mpango wa 'Pamoja Hadi Mwisho' atanufaika yeye mwenyewe, mwenza wake, watoto (nafasi nne kwa ajili ya watoto wenye umri kuanzia miaka (0 - 21)), wazazi, na wakwe," alisema.

Juma Patrice, Meneja wa Bima kutoka Alliance Life Assurance alisema kuwa endapo mwanachama au mtegemezi wa mwanachama (mwenza au watoto au wazazi au wakwe) atafariki kutokana na ajali au ugonjwa, mkono wa pole wa rambirambi wa kiasi cha Sh. milioni 3.5 hadi Sh. milioni 6 au kiasi cha Sh. 500,000 hadi Sh. milioni 5 kitatolewa kwa familia ya mwanachama aliyefariki au kwa mwanachama aliyefiwa na mtoto au mwenza au mzazi au mkwe. Rambirambi hii itatolewa ndani ya saa 72, baada ya kupokea nyaraka zote za madai.

## HABARI MICHEZO

# OFISA JESHI JWTZ ATUNUKIWA NISHANI UTENDAJI BORA CISM

**Na Meja Selemani Semunyu**

MKURUGENZI wa Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM), Kanali Joseph Bakari, ametunukiwa nishani ya "Officer" kwa kutambua moyo wa kujituma, bidii na juhudi zake katika kuendelea michezo jeshini ikiwa ni sehemu ya kutekeleza malengo ya CISM kwa kutumia shughuli za michezo na utimamu wa mwili kueneza amani duniani.

Kwa Mujibu wa Mtandao wa CISM, nishani hiyo ya Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (International Military Sports Council -CISM), yenye makao yake makuu jijini Brussels, Ubelgiji, imetolewa wakati wa mkutano mkuu wa mwaka ulioanza Mei Mosi hadi Mei 9, mwaka huu, jijini Lima, Peru.

Mkutano huo ambao ni wa kwanza kwa wanachama kukutana uso kwa uso tangu mwaka 2019 kutokana na janga la UVIKO-19, uliohudhuriwa na nchi wanachama 65 kutoka katika mabara ya Afrika, Amerika, Asia na Ulaya.

**Kanali Bakari, alivishwa nisha ni hiyo na rais wa baraza hilo, Brig Gen Herve Piccilliro, kuto ka Ufaransa mbele ya wajumbe takriban 400 waliohudhuria mkutano huo kutoka pande zote duniani.**

Kwa sasa Kanali Bakari anakuwa ni Mtanzania pekee kupata nishani ya pili ya utendaji bora katika baraza hilo. Mwaka 2008 aliwahi kutunukiwa nishani iitwayo 'Grand Knight' nchini Suriname mjini Paramaribo kutokana na juhudi zake za kukuza vipaji vya michezo kupitia Kituo cha Twalipo Youth Sports ambacho alikianzisha.

Baraza la Michezo ya Majeshi, hutunuku nishani kwa yeyote ambaye kwa matendo yake ametekeleza malengo ya CISM na kwa utendaji wake amechangia maendeleo ya michezo kwa majeshi ya nchi wanachama.

Mbali na Kanali Bakari, baadhi ya wanajeshi wengine waliotunukiwa nishani siku hiyo katika madaraja mbalimbali ni pamoja na Meja Gen Katirima Manoni Phinehas (Uganda), Kanali Moussa Moise Keita (Guinea), Mteule Bongseok Kim (USA), Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Peru, Luteni Jenerali David Guillermo Ojeda Parra, Kapteni wa Wanamaji Spyridon Andriopoulos (Ugiriki), Meja Jenerali Grancisco Javier Costa Gallegos (Peru), Luteni Kanali Lars Gerhardsson (Sweden), Luteni Kanali Jan Van den Dool (Uholanzi).

**TUMESHIRIKI...**




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Absa Tanzania, wakicheza kwa furaha baada ya kushiriki mbio za Dar City Marathon jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba Queens bado mbili bingwa*

**Na Adam Fungamwango**

IWAPO itashinda mechi mbili kati ya nne zilizosalia nazo kwenye Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu, timu ya Simba Queens itatawazwa kuwa Mabingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo.

Hiyo ni baada ya juzi kuitwanga timu ngumu ya Fountain Gate Girls mabao 4-0 katika Uwanja wa Fountain Gate.

Yalikuwa ni mabao mawili ya straika hatari wa Kirundi, Asha Djaffar, Aisha Juma akifunga mawili na Jackline Albart moja.

Simba Queens imefikisha jumla ya pointi 51, ambapo kama ikishinda mechi mbili tu itafikisha jumla ya pointi 57 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile.

Fountain Gate Girls, ndiyo timu iliyoonekana ni hatari kwenye mbio za ubingwa na Simba, lakini sasa imebaki na pointi 44 na kama itashinda mechi nne ambazo imesalia nazo itafikisha jumla ya pointi 56.

Baada ya ushindi huo, wachezaji wa timu hiyo walionekana kushangilia kama vile tayari wametwaa ubingwa kwenye mechi hiyo iliyoonekana kama ni fainali, kwani ndiyo timu pekee iliyoonekana wanaihofia, ikishika nafasi ya pili kwa muda mrefu, ikiwa imepoteza mechi mbili tu, ambazo zote imefungwa na Simba Queens mzunguko wa kwanza na wa pili.

Simba Queens imefunga mabao 85 na kufungwa sita, huku Fountain Gate Girls ikiendelea kuwa ya pili kwa pointi 44, mabao 61, ikifungwa 18.

Yanga Princess nayo baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ruvuma Queens, pia imefikisha pointi 44, ingawa kama wenzao Fountain Gate Girls, wakishinda mechi nne zilizobaki watafikisha pointi 56 tu.

Ni timu 12 tu zinazoshiriki ligi hiyo na tayari kila timu imeshacheza mechi 18.

## Kaseba mwenyekiti TPBA, Mbabe chali

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BINGWA wa zamani wa mchezo wa ngumi na mateke (Kickboxing), Japhet Kaseba, ameshinda nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Umoja wa Mabondia wa Ngumi za Kulipwa (TPBA), huku Bondia Abdallah Pazzi 'Dullah Mbabe' akipigwa chini katika kinyang'anyiro cha nafasi ya ujumbe.

Katika uchanguzi huo uliofanyika juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kusimamiwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Kaseba alitangazwa mshindi baada ya kupata kura 26 wakati mpinzani wake, Mada Maugo akipata kura 16.

Kwa upande wa wajumbe Dulla Mbabe aliambulia kura 20, wakati Francis Miyeyusho akishinda kwa kura 24 na Fatma Yazidu akipata kura 25.

Akizungumza na gazeti hili jana katika uchaguzi huo, Ofisa Michezo wa BMT, Allen Alex, alisema viongozi wa TPBRC wanatakiwa kuwa makini na kuhakikisha wanatatua changamoto zinazojitokeza katika mchezo huo.

Alisema katika ngumi kuna changamoto nyingi sana ambazo viongozi wapya wanatakiwa kuzifanyia kazi ili kuhakikisha mchezo huo unakuwa imara na kurejea katika heshima ya taifa.

## Taifa Wanawake Zanzibar waiwinda Cecafa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Wanawake Zanzibar, Abdulmutik Ali, ameita wachezaji 30 watakaounda kikosi chake kuelekea michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Mei 22, mwaka huu, nchini Uganda.

Timu hiyo ilianza mazoezi rasmi tangu Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Amaan Kisiwani Unguja.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Ali alisema kutokana na muda wa maandalizi kuwa mdogo timu hiyo imeanza kufanya mazoezi kila asubuhi na baadhi ya siku watafanya mazoezi ya ufukweni jioni.

Alisema wachezaji wote aliowaita ameanza nao vizuri na ana matumaini makubwa ya kufanya vizuri katika michuano hiyo.

"Kwa hatua ya awali, tumewaita wachezaji 30 ambao tumeanza nao mazoezi, lakini baada ya wiki moja kabla ya kuelekea katika mashindano tutakuwa na wachezaji 20," alisema.


## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### HAALAND HUYO MAN CITY

MANCHESTER City wiki ijayo huenda ikatangaza usajili wake ghali wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. ***(Sun)***

#### TCHOUAMENI AGOMBEWA



LIVERPOOL inaongoza mbio zinazozijumuisha pia klabu za Real Madrid na Chelsea katika kuwania saini ya kiungo Mfaransa anayecheza Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. ***(Marca via Metro)***

#### ARSENAL KUMKOSA MARTINEZ

ARSENAL inaweza kugonga mwamba katika mpango wake wa kumsajili mshambuliaji Muargentina Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24 kwani Inter Milan inaonekana haitamuuza. ***(Gazetta Dello Sport)***

#### NKUNKU AWINDWA EPL




KLABU za Arsenal, Chelsea na Manchester United zinamwania kiungo wa RB Leipzig, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24 msimu huu. ***(Football.London)***

#### LAIMER KUTUA BAYERN

BAYERN Munich inaandaa ofa ya kwanza ya pauni milioni 15 ili kuanza mazungumzo na RB Leipzig kwa ajili ya kiungo wake, Konrad Laimer mwenye umri wa miaka 25. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

#### BECKHAM NA RONALDO



KIUNGO wa zamani wa Manchester United, David Beckham anatumai Cristiano Ronaldo, 37, atabaki Old Trafford msimu ujao. ***(Talksport)***

#### RUTTEN AMEKATALIA HAG

KIUNGO wa zamani wa Uholanzi, Fred Rutten, amefichua kwamba amekataa ofa ya kuwa mmoja wa wasaidizi wa Erik ten Hag pale Manchester United. ***(Guardian)***

#### BARAK AWANIWA SPURS




KLABU ya Tottenham Hotspur itakabiliana na upinzani kutoka klabu za Bundesliga na Serie A katika mbio za kumsajili kiungo wa Hellas Verona kutoka Czech, Antonin Barak mwenye umri wa miaka 27. ***(Inside Futbal)***

#### RAMSAY ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ina matumaini ya kuipiku Leeds United katika usajili wa pauni milioni nne wa mlinzi wa Aberdeen na Scotland, Calvin Ramsay, 19. Kinda huyo anaandaliwa kumsaidia Trent Alexander-Arnold. ***(Goal)***

#### BOAS KUINOA MOROCCO



KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Andre Villas-Boas anaweza kuwa kocha wa Morocco, na kufungua milango ya kurejea kwa Hakim Ziyech kwenye timu kikosi cha taifa. ***(Le360 via Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# CITY KUWAKOSA MABEKI WA3 MBIO ZA UBINGWA

Katika hali hii si shida, ikiwa Rodri atalazimika kucheza katika nafasi hiyo au...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amefichua kwamba, Manchester City itawakosa mabeki watatu muhimu katika mbio za mwisho za kuwania taji la Ligi Kuu England na akatania Phil Foden atalazimika kucheza kama beki.

**Kyle Walker, John Stones na Ruben Dias hawatarudi uwanjani kwa kipindi kilichobaki msimu huu kutokana na kuumia, wakati Dias alilazimika kutoka kipindi cha mapumziko dhidi ya Newcastle United Jumapili baada ya kuumia misuli.**

City walishinda mabao 5-0 na walikuwa na nguvu kubwa dhidi ya Newcastle, lakini kuna mechi za ugenini dhidi ya Wolves na West Ham kabla ya kumaliza msimu wao nyumbani kwa Aston Villa.

Man City sasa wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya Liverpool wanaoshika nafasi ya pili.

Aymeric Laporte alicheza kwa ushirikiano na mkongwe Fernandinho katika kipindi cha pili dhidi ya Newcastle.

"Katika hali hii si shida. Ikiwa Rodri atalazimika kucheza katika nafasi hiyo si shida, au ikiwa ni mtu kutoka akademi," alisema Guardiola.

Awali Guardiola aliiambia Sky Sports: "Phil Foden atalazimika kucheza kama beki wa kati."

Alipoulizwa kama hilo linaweza kutokea kweli, Guardiola alijibu: "Hapana."

Guardiola alisema City walikuwa "bora" na walionyesha mchezo "bora" dhidi ya Newcastle, siku nne baada ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid.

"Tumekuwa tukifanya hivi kwa miaka mitano kila baada ya siku tatu, ikiwa kuna watu wanatutilia shaka ni kwa sababu bado hawajui timu hii na ina uwezo gani.

"Sizungumzi juu ya kushinda au kushindwa. Si mchana mmoja au usiku mmoja. Ni miaka mingapi, kuwa huko kila siku tatu, kila wakati."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ASTON VILLA
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 6.13
X | 4.55
2 | 1.43

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BECKHAM ATAKA RONALDO ABAKI MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester United, David Beckham, amekiri mabadiliko yanahitajika pale Old Trafford, lakini anatumai Cristiano Ronaldo atabaki kuwa sehemu ya mipango ya 'Mashetani Wekundu' hao.

United ya Ralf Rangnick ilikutana na kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Brighton, Jumamosi na hiyo maana yake ni kwamba, wameruhusu mabao zaidi (56) msimu huu kuliko msimu wowote wa Ligi Kuu England.

Kocha wa Ajax, Erik ten Hag atachukua nafasi ya Rangnick mwishoni mwa msimu huu, lakini Mholanzi huyo atapewa kazi kubwa ya kukijenga upya kikosi, huku wachezaji wengi wakitarajiwa kuondoka.

Inasemekana kwamba Paul Pogba analengwa na majirani zao, Manchester City mkataba wake utakapomalizika Juni, huku mustakabali wa Ronaldo ukiwa haujulikani.

Ronaldo amefunga mabao tisa kati ya 13 ya mwisho ya ligi ya United katika mechi 11. Hata hivyo, maswali yanaendelea kuhusu ushawishi wa mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid katika harakati za United.

Na Beckham anataka Ronaldo aonekane kama sehemu muhimu ya mipango ya Ten Hag msimu ujao.

"Ni wazi Cristiano ni mmoja wa wachezaji bora zaidi ya miaka 15 iliyopita, akiwa na Leo (Messi)," alisema Beckham akiiambia Sky Sports.



# 'Tutapambania nne bor

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesisitiza kuwa Atletico Madrid bado wana kazi kubwa ya kufanya kama wanataka kumaliza katika nafasi nne za juu za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Atletico waliwashinda wapinzani wao wakubwa, Real Madrid bao 1-0 wakiwa Wanda Metropolitano Jumapili na kusonga mbele kwa pointi sita dhidi ya Real Betis walio katika nafasi ya tano huku kukiwa na mechi tatu kabla ya msimu kumalizika.

Mkwaju wa penalti wa Yannick Carrasco dakika ya 40, ulitosha kwa Atletico kupata ushindi huo.

'Los Rojiblancos' hao wanaweza kufuzu kwa mara ya 10 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama watapata pointi tatu dhidi ya Elche Jumatano, lakini Simeone amesema wa akiwa kupambana.

"Zimesalia mechi t Kila mmoja anashind kumaliza nafasi ya nne haitakuwa rahisi," alis akiiambia Movistar.

"Lakini kwa kweli h hatua kali na ya maan kwetu.

"Tulicheza mchezo bao tulitaka kucheza. lipata nafasi nyingi, la hatukuweza kutumia vu na hilo lilitusukuma.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# KAPOMBE ACHEKELEA MECHI 100, BOCCO AKIFUNGA DK. 522

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, amesema limekuwa ni jambo la furaha kwake kutimiza mechi 100 alizocheza ndani ya klabu hiyo, tangu ajiunge tena akitokea Azam FC, akieleza tamu na chungu alizokutana nazo.

Kapombe ambaye alijiunga na Simba mwaka 2017, akitokea Azam FC, amesema halikuwa jambo rahisi kutoka Azam FC kutokana na mambo mengi waliyomfanyia, lakini mwisho wa siku maisha ni kama mzunguko, ilibidi arejee kwenye timu yake ya zamani ya Simba.

"Nashukuru kwangu ni jambo la furaha, si jambo dogo kufikisha mechi 100, namshukuru Mungu nimekuwa nacheza miaka yote kwa kiwango kikubwa, wapo waliocheza kwa miaka kama hii mitano sasa, lakini hawakufikisha michezo kama hii. Nawashukuru walimu wangu wote waliopita, wachezaji na familia yangu, muhimu hapa ni kwamba nimetoa mchango mkubwa kwenye klabu na kutwaa mataji mbalimbali, ingawa ugumu niliokutana nao ilikuwa kuondoka Azam FC. Haikuwa rahisi kwa sababu walinifanyia vitu vingi vizuri," alisema.

Hata hivyo, mwaka 2017 haikuwa mara ya kwanza kwa mchezaji huyo kuichezea Simba, kwani awali alijiunga na timu hiyo akitokea Polisi Morogoro na kuingia 2011, hadi 2013 alipokwenda nchini Ufaransa kwenye Klabu ya AS Cannes, alipodumu kwa mwaka mmoja, kabla ya kurejea na kujiunga na Azam mwaka 2014 hadi 2017, aliporejea kwenye klabu yake ya zamani, Simba.

Wakati huo huo, straika wa Simba, John Bocco amefunga bao lake la kwanza msimu huu kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bocco alifungua akaunti yake kwenye mechi hiyo, akipachika bao la tatu dakika ya 82, kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting juzi usiku, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu yake ikishinda kwa mabao 4-1, akisubiri kufanya hivyo kwa dakika ya 522, siku 295 na michezo 13.




Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Ruvu Shooting juzi usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# *DTB yaanza mkwara Ligi Kuu Bara*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupanda Ligi Kuu kuelekea msimu ujao, Klabu ya DTB imesema ina malengo makubwa kwa msimu wa 2022/23, hivyo imepanga kufanya usajili wa nguvu, ikitamba kuwa hakuna mchezaji ambaye ikimtaka ikamkosa.

Mwishoni mwa wiki, timu hiyo ilikuwa ya kwanza kupanda Ligi Kuu baada ya kuitwanga Pamba FC kutoka Mwanza bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam katika Ligi ya Championship, na kufikisha pointi 65, ambazo kimahesabu tayari imepanda Ligi Kuu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Muhibu Kanu, amesema kama walivyofanya usajili wa kutisha kwa ajili ya Ligi ya Champiionship, pia watafanya hivyo kuelekea Ligi Kuu, lakini wakija na mapinduzi makubwa yatakayozitetemesha klabu zinazoitwa au kujiita kubwa.

"Tunashukuru kwa hiki tulichokipata, tumepanda tukicheza kwenye ligi ambayo kwa mara ya kwanza ilikuwa ni ya mkondo mmoja, tofauti na zamani ilivyokuwa ya makundi, ilikuwa pia na changamoto nyingi. Lakini inaonyesha kuwa mpira hauna njia ya mkato.

"Nilipoingia niliamua kufanya usajili wa wachezaji mahiri kama kina Amissi Tambwe, David Mwantika, Nicolaus Gyan, James Kotei, Yusuph Mlipili, Juma Abdul na wengineo ambao wametuwezesha kufika hapa tulipo. Bado tuna mechi mbili, siku ya mwisho nitaweka hadharani mikakati yangu kuelekea kwenye Ligi Kuu msimu ujao, ila tutafanya usajili wa nguvu na hakuna mchezaji ambaye tutamtaka halafu tumkose," alisema Muhibu.

Wakati DTB ikipanda moja kwa moja, Ihefu inayoshika nafasi ya pili kwa pointi 62, ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kurejea Ligi Kuu, kama itafanya vema kwenye mechi ilizosalia. Ihefu, yenye maskani yake Mbarali, Mbeya, iliteremka daraja msimu uliopita.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 10/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4149 | FC Shevardeni vs FC Spaeri | 1.84 | 3.75 | 3.45 |
| 16:00 | 2516 | FC Petaling Jaya City vs Kedah | 5.25 | 3.99 | 1.52 |
| 16:00 | 3985 | Mbeya City vs Azam | 2.71 | 2.71 | 2.76 |
| 16:30 | 2540 | Dinamo Moscow vs FC Alania Vladikavkaz | 1.32 | 4.76 | 7.57 |
| 17:00 | 3610 | Neftchi Fargona vs FC Olimpik | 1.58 | 3.45 | 5.63 |
| 17:00 | 4181 | Bunyodkor vs Metallurg Bekabad | 1.52 | 3.76 | 5.66 |
| 17:00 | 5557 | AL Urooba vs Baniyas | 4.47 | 3.79 | 1.63 |
| 17:00 | 5660 | FK Tukums 2000/Tss vs FK Auda | 5.27 | 3.81 | 1.54 |
| 17:30 | 5133 | Gokulam Kerala FC vs Sreenidi Deccan FC | 1.64 | 3.70 | 4.58 |
| 18:00 | 2200 | Halmstads BK U21 vs Mjallby AIF U21 | 1.59 | 4.66 | 3.88 |
| 18:00 | 3529 | FK Liepaja vs Spartaks Jurmala | 1.04 | 9.37 | 28.29 |
| 18:00 | 3874 | CR Belouizdad vs RC Arbaa | 1.34 | 4.60 | 9.40 |
| 18:10 | 1126 | Nizwa vs AL Etihad | 2.68 | 2.83 | 2.68 |
| 18:10 | 2003 | Oman Club vs Sohar Club | 2.73 | 2.83 | 2.63 |
| 18:10 | 2270 | Al Seeb vs AL Musanaa | 1.48 | 3.89 | 6.03 |
| 18:10 | 4587 | Dhofar Salalah vs Al Nasr Salalah | 1.79 | 3.20 | 4.36 |
| 18:10 | 5378 | Muscat Club vs Bahla | 2.53 | 2.82 | 2.87 |
| 18:10 | 5577 | Saham Club vs Al Suwaiq | 4.49 | 3.07 | 1.81 |
| 18:55 | 4033 | Al Qadisiyah vs Al Orubah | 2.05 | 3.10 | 3.85 |
| 19:00 | 1521 | Kiffen vs Nurmijarven Jalkapalloseura | 1.62 | 3.99 | 4.28 |
| 19:00 | 4532 | SK Super Nova vs FC Riga | 13.59 | 6.21 | 1.16 |
| 19:30 | 1924 | Universitatea Cluj vs Hermanstadt | 2.24 | 2.82 | 3.35 |
| 19:30 | 4969 | Ceramica Cleopatra vs El Gouna | 2.14 | 2.80 | 4.00 |
| 19:45 | 3953 | NAC Breda vs ADO Den Haag | 2.19 | 3.47 | 2.98 |
| 19:45 | 5379 | Al Sharjah SC vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.51 | 4.08 | 5.24 |
| 19:45 | 5627 | Mechelen vs KAA Gent | 3.59 | 3.64 | 1.92 |
| 20:00 | 1866 | Baumit Jablonec vs Bohemians | 1.75 | 3.53 | 4.84 |
| 20:00 | 3135 | Jonkopings Sodra vs Landskrona Bois | 2.04 | 3.48 | 3.53 |
| 20:00 | 3683 | MFK Karvina vs Teplice | 2.76 | 3.26 | 2.56 |
| 20:00 | 4401 | Pardubice vs Zlin | 2.05 | 3.49 | 3.49 |
| 20:00 | 5906 | Valencia vs Betis | 3.70 | 3.45 | 1.96 |
| 20:30 | 1761 | Kayserispor vs Trabzonspor | 3.32 | 3.27 | 2.03 |
| 20:30 | 1839 | Neuchatel Xamax vs Yverdon-Sport FC | 2.15 | 3.49 | 2.86 |
| 20:30 | 2278 | Hapoel Tel Aviv vs Hapoel Beer Sheva | 3.56 | 3.27 | 1.95 |
| 20:30 | 4045 | SC Kriens vs FC Vaduz | 4.49 | 4.10 | 1.58 |
| 20:30 | 4594 | FC Thun vs FC Schaffhausen | 2.68 | 3.71 | 2.19 |
| 20:30 | 5077 | Maccabi Haifa vs Maccabi Tel Aviv | 1.92 | 3.40 | 3.50 |
| 20:30 | 5274 | Maccabi Netanya vs Bnei Sakhnin | 1.70 | 3.40 | 4.57 |
| 21:00 | 2406 | Granada vs Athletic Bilbao | 3.71 | 3.41 | 1.97 |
| 21:05 | 5222 | Inverness vs Arbroath | 2.23 | 3.32 | 3.07 |
| 21:30 | 1379 | Edinburgh City vs Annan Athletic | 2.31 | 3.36 | 2.82 |
| 21:30 | 1461 | BSC Young Boys vs St. Gallen | 1.53 | 4.50 | 5.00 |
| 21:45 | 2105 | Dundee FC vs Hibernian | 3.59 | 3.29 | 2.03 |
| 21:45 | 4287 | Grimsby vs Boreham Wood | 2.09 | 3.25 | 3.35 |
| 21:45 | 5595 | Bromley vs Altrincham | 2.05 | 3.45 | 3.25 |
| 22:00 | 2574 | SBV Excelsior vs Roda Kerkrade | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 22:00 | 3939 | Aston Villa vs Liverpool | 6.13 | 4.55 | 1.43 |
| 22:00 | 4323 | Zamalek vs Enppi Club | 1.58 | 3.55 | 6.21 |
| 22:00 | 4931 | Racing Genk vs Charleroi | 1.64 | 4.07 | 4.57 |
| 22:30 | 2675 | Barcelona vs Celta Vigo | 1.43 | 4.69 | 6.36 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Mei 10, 2022
Nipashe



## City kuwakosa mabeki watatu
UKURASA 21

UMETISHA...




Makocha wa Simba, Kocha Mkuu, Pablo Franco (kushoto) na Msaidizi wake, Selemani Matola (kulia), wakimkabidhi beki wa timu hiyo, Shomari Kapombe jezi ya kutimiza mechi 100 tangu ajiunge na timu hiyo mwaka 2017 akitokea Azam FC. Makabidhiano hayo yalifanyika juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting iliyomalizika kwa Simba kushinda 4-1. **Habari UK. 23. PICHA: SIMBA.**

# Pablo afunguka tetesi kutua Orlando Pirates

**Na Saada Akida**

## ●●● Pia asema bado mbio za ubingwa zipo wazi, Mkwasa naye...

HUKU tetesi zikizidi kuvuma kuwa Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amepata ofa ya kwenda kuinoa Orlando Pirates ya Afrika Kusini, Nipashe limebisha hodi kwa kocha huyo kutaka kujua ukweli kuhusu suala hilo na msimamo wake.

**Orlando Pirates kwa sasa ipo chini ya kocha wa muda, Mandla Ncikazi, ambaye anaonekana kukalia kuti kavu kutokana na mashabiki wa timu hiyo kutomkubali, sababu ikiwa ni mwenendo mbaya kwenye Ligi Kuu Afrika Kusini, wakati huu ikiwa nafasi ya sita na alama zake 40 baada ya mechi 27.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, ambayo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 4-1, Pablo alipata kigugumizi kujibu kutakiwa na Orlando Pirates na timu nyingine zinazodaiwa kuhitaji huduma yake.

"Hizo ni tetesi kwa sasa siwezi kulizungumzia suala hilo kwa sababu mimi ni mwajiriwa wa klabu ya Simba," alisema kwa kifupi kocha huyo raia wa Hispania.

Kuhusu mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Pablo aliweka wazi kuwa bado hawajakata tamaa kwa sababu wana mechi nane zilizobaki kabla ya msimu kumalizika.

Pablo alisema ingawa wapo nyuma kwa alama 10 dhidi ya vinara Yanga, lakini kwa kuwa bado wana idadi kubwa ya michezo iliyobaki lolote linaweza kutokea. Alisema baada ya kutoka sare dhidi ya Yanga katika mchezo uliopita walijiweka katika mazingira magumu ya kutetea ubingwa kutokana na ratiba kubana, lakini hata kwa wanaoongoza lolote linaweza kutokea.

"Kama nilivyowahi kusema huko nyuma mbio za ubingwa bado zipo wazi, tupo nyuma kwa pointi 10, lakini kama wanaongoza wataendelea kudondosha pointi na sisi tukishinda zetu, tunaweza kutetea ubingwa.

"Nimefurahi kwa ushindi huu mnono, mchezo ulikuwa mzuri tumetengeneza nafasi nyingi kipindi cha kwanza, lakini hatukuzitumia vizuri, tulivyorudi cha pili tulirekebisha makosa na kufanikisha ushindi huu," alisema Pablo huku akifunguka kuwa amefurahi kuona mshambuliaji wake, John Bocco amepata bao lake la kwanza jambo ambalo limerejesha morali ndani ya timu hiyo na mchezaji husika.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, alisema ulikuwa mchezo mzuri, lakini wamepoteza kutokana na uzoefu wa kikosi cha Simba, lakini wanajipanga kwa ajili ya michezo iliyosalia ya Ligi Kuu Bara.

"Tulikuwa vizuri kipindi cha kwanza kama tungeendelea na ubora ule tungefanya kitu, kipindi cha pili wachezaji walikuwa wamechoka wakawa wanashindwa kukaba, bado tuna nafasi ya kushinda katika michezo iliyosalia hatuwezi kushindana na Simba ni timu kubwa iliyokaa pamoja muda mrefu.

"Simba wametushinda kutokana na uzoefu wao, sisi tuna timu changa ambayo inajipanga, pointi moja ya Yanga tuliyopata Kigoma imetuponza tumetembea kilomita 2800, hivyo tulikuwa na uchovu japokuwa siwezi kusema hii ndiyo iliyotugharimu," alisema Mkwasa.

## Beckham ataka Ronaldo abaki Manchester Utd

**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester United, David Beckham, amekiri mabadiliko yanahitajika pale Old Trafford, lakini anatumai Cristiano Ronaldo atabaki kuwa sehemu ya mipango ya 'Mashetani Wekundu' hao...




HABARI UK. 22

## DTB FC yaanza vitisho Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupanda Ligi Kuu kuelekea msimu ujao, Klabu ya DTB imesema ina malengo makubwa kwa msimu wa 2022/23, hivyo imepanga kufanya usajili wa nguvu, ikitamba kuwa hakuna mchezaji ambaye ikimtaka ikamkosa.



HABARI UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >